# Nipashe

Jumanne Novemba 17, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580402

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

**EWURA,** LATRA kushirikiana kuboresha usafirishaji mafuta

UKURASA 3



**AFUNGWA** jela miaka 30, viboko 12 kwa kubaka

UKURASA 4



**De Bruyne ateta kubaki Man City**

# JPM ataja umri mrithi wake mwaka 2025

• **Ataja** sababu za kuchelewa kuunda Baraza la Mawaziri, aeleza kuwateua Mpango, Kabudi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Dk. John Magufuli akimwapisha Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu, katika hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma jana. Waziri Mkuu Majaliwa alipitishwa na Bunge wiki iliyopita. **PICHA: IKULU**

## Mpango: Umaskini bado ni mkubwa

UKURASA 3

## PM acharuka saruji kupaa, atoa siku 4 apate ripoti

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

MICHEZO STARS, TUNISIA KUAMUA AFCON UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM ataja sifa za mrithi wake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Dk. John Magufuli ametaja sifa za mtu atakayefaa kumrithi, huku akieleza kuwa Watanzania wanataka mtu kijana.

Pia, ameeleza sababu za kuchelewa kutangaza Baraza la Mawaziri na kuwataka wabunge kushusha presha ya kuteuliwa kwa kuwa kazi waliyoomba ni ubunge na si uwaziri.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino baada ya kumwapisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mawaziri wawili, Rais Magufuli alisema haiwezekani kupendekeza kwenye kikao cha Kamati Kuu ya CCM kuchagua mtu mwenye umri wa miaka 60.

"Maneno mengine yanaumiza, lakini mjiandae kisaikolojia kusudi msipoteze fedha zenu, najua haya mambo ni magumu huo ndio ukweli, Kikwete wakati anaondoka alisema hataona rais anayemzidi umri, sasa mwangalie mimi nina umri gani nitakapokuwa namaliza ndio ujipimie kwenye umri pale," alisema.

Alisema asilimia 65 ya Watanzania ni vijana na imemsaidia Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kushinda kwa kuwa wapigakura kwa sasa ni vijana.

"Huo ndio ukweli, huwezi kuwapelekea wapigakura mtu ambaye si saizi yao, maneno yanauma, lakini ndio hivyo," alisema.

**PRESHA WABUNGE**

"Sikuwa na haraka ya kuteua Baraza la Mawaziri na nyie wabunge ni mashahidi, mwaka huu tuna wabunge zaidi ya 350 na bado wa nafasi 10, sikutaka kuteua haraka na ningewaomba wabunge presha mzishushe kwa sababu kazi tuliyoomba ni ubunge wala sio uwaziri," alisema.

Aliwakumbusha kuwa walienda kuomba ubunge na watawatumikia wananchi na kukabidhiwa Ilani ya uchaguzi yenye kurasa 303.

"Sasa mengine yanatoka wapi? Nafasi za uwaziri na naibu waziri haziwezi kufika 30, sasa katika watu 350 hata ungekuwa wewe unateua ungepata shida kubwa, kwa hiyo lazima nicheki jina kwa jina, factors (sababu) nyingi, na wakati mwingine unatafuta factors nyingine ili umtoe," alisema.

Alisema haiwezekani kukawa na wabunge kwenye mkoa mmoja watano na kueleza kuwa hiyo ni miongoni mwa mambo ya kuangalia ya kuwapo na mgawanyo.

"Kuna factor kubwa na kazi ni ngumu, ni lazima uwe fair (haki) na umtangulize Mungu, kwamba anayestahili usije ukamwonea, kwa hiyo nawaomba ndugu zangu mnisamehe sana kwamba inachukua muda mrefu," alisema.

Alieleza kuwa mwaka 2015 ilikuwa ni rahisi kwa sababu wabunge wa CCM walikuwa wachache na idadi ya kucheza nayo ilikuwa ndogo.

**SABABU MAWAZIRI WAWILI**

"Hawa wawili sio ndio maarufu sana kuliko waliobaki, miaka ya nyuma niliwateua hawakuwa na majimbo na niliwaambia waende kwenye majimbo, lakini nikaona nitachelewa kidogo kuteua Baraza la Mawaziri na wabunge lazima mlipwe mishahara, posho na mishahara ya wafanyakazi, miradi ya maji na kila kitu ni lazima tuwe na Waziri wa Fedha," alisema.

Alifafanua: "Kwa sababu nilijua fedha tutahitaji haiwezi kusubiri miezi mitatu au minne, ndio maana nikaangalia, nikasema huyu Mpango kabla sijamteua alikuwa Kamishna wa TRA ndio alikuwa mtu wa kwanza kukusanya mapato kutoka Sh. bilioni 850 hadi trilioni 1.2, nikamteua kuwa Waziri wa Fedha na amekuwa pale na uchumi umeendelea kupanda."

Kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje, Rais Magufuli alisema aliamua kumteua Prof. Kabudi kwa kuwa nchi haiwezi kukaa bila mtu wa kuisemea.

"Hatuwezi kukaa bila mtu wa kutusemea tukaendelea kutukanwa, watu wanatengeneza majambo yao hayapati majibu, ndio maana nikasema huyu kwa kuwa alimudu kazi yake nikasema aendelee kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, wapo wengi waliomudu nafasi zao, lakini niliona nijiridhishe kwanza," alisema.

Alisema wasaidizi wake walimpelekea ushauri kuhusu Wizara ya Ulinzi na Mambo ya Ndani, lakini hakuwajibu.

"Sikuwajibu kwa sababu si lazima kuwa na Waziri wa Ulinzi, CDF akiwa na tatizo au akitaka kupigana wala haendi kwa Waziri wa Ulinzi, anakwenda kwa Rais ambaye ndiye kamanda mkuu, kwa hiyo ushauri ule hata sikusikiliza, ukihitaji polisi waende kufanya kazi mahali popote haihitaji Waziri wa Mambo ya Ndani, IGP atafoka watu watatoka," alisema.

Akizungumzia wizara nyingine, alisema zitasimama kwenye uteuzi hadi ajiridhishe.

"Wapo makatibu wakuu wafanye kazi na wajibu wao, kwa hiyo ninawaomba sana wabunge nawapenda sana na wote mna sifa, kitakachofanyika ni randomization tu, wote supa na tuliwapitisha kwenye Kamati Kuu na Halmashauri Kuu na wananchi wakawapa kura za kutosha ndio maana nimeona tupeleke taratibu na si kwa haraka," alisema.

Hata hivyo, alisema atakaa na viongozi wenzake akiwamo na Rais wa Zanzibar ili kushauriana kwenye uteuzi.

"Nitakaa na Rais wa Zanzibar kwa kuwa yawezekana ninayetaka kumteua na yeye anataka kumteua Zanzibar, kwa hiyo ni suala ambalo halihitaji haraka, maneno ni mengi, kwa waganga nendeni shauri yenu, wengine watawapaka mikosi," aliwaasa.

Aliwashauri kwenda kanisani na msikitini kumwomba Mungu ndipo kwenye baraka nzuri.

**AMPA SOMO MAJALIWA**

Alimpongeza Waziri Mkuu Majaliwa na kusema anashangaa kwenye vyombo vya habari watu wakishangilia kuwa amepewa miaka mingine mitano bila kujua kama amewaambia atakaa miaka hiyo.

"Nataka niwaambie na nimwambie Majaliwa kazi ya uwaziri mkuu haina guarantee (kipindi maalum), nilitaka nilizungumze hili Waziri Mkuu aelewe, itategemea na performance (utendaji) wake kwa hiyo tumwombee, ili angalau afikie rekodi ya Waziri Mkuu mstaafu Fredrick Sumaye," alisema.

Alisema wanasiasa wana tabia ya kufurahi, lakini nafasi hiyo sio ya kudumu na kuwataka wateuliwa kutambua uteuzi unategemea na namna kazi ilivyofanyika.

"Wananchi wametukopa imani, lazima tukafanye makubwa sana, nampongeza Waziri Mkuu miaka mitano iliyopita alifanya kazi nzuri, miaka hii mitano Waziri Mkuu ni migumu nitakutuma sana, mwaka huu sio raha."

Kwa upande wake, Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu, alisema viongozi aliowarudisha kwenye nyadhifa zao akiwamo yeye hawakuwa na kazi rahisi kwa kuwa walikuwa wakilia kutokana na Rais Magufuli kuwanyoosha.

"Tulipoanza nawe ilikuwa kazi ngumu, ulikuwa unatuona tulikuwa tunalia kila siku, ukija kwangu nilikuwa nasema eeh mwaka huu, kina Kassim wote hawa, lakini uliendelea kutunyoosha, tumenyooka, miaka miwili ya kwanza tulinyooka, miaka mitatu iliyofuata tulifanya kazi kweli na ukawa na imani juu yetu," alisema.

"Tunasubiri baraza jipya la mawaziri, lakini sisi tutawanyoosha, mwenzetu utakaowateua wewe fikiria mengine makubwa na si utakaowateua."

Naye Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisisitiza ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kutimiza waliyokubaliana katika masuala mbalimbali likiwamo la uchumi ambao unategemea pande zote mbili.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, wakila kiapo cha uadilifu baada ya kuapishwa kuwa mawaziri na Rais Dk. John Magufuli, katika hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# PM atoa siku 4 apewe ripoti kupanda saruji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema anaanza kazi kwa kushughulikia suala la upandaji wa bei ya saruji nchini, huku akitoa siku nne kwa wakuu wa mikoa kukagua viwanda na mawakala na kuwasilisha taarifa ya sababu za kupanda kwa bei hiyo.

Hatua hiyo imetokana na hivi karibuni bei ya bidhaa hiyo kupanda kwa viwango tofauti kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino baada ya kuapishwa na Rais Dk. John Magufuli, alisema kuna watu wamejisahau wakidhani serikali ipo kwenye uchaguzi na haiwezi kufanya lolote jambo ambalo si kweli.

Alisema bei hiyo imepanda bila sababu yoyote ya msingi kwa kuwa serikali haijaongeza kodi, miundombinu, gesi, makaa ya mawe yapo mengi na nguvu kazi ipo.

"Tunahitaji maelezo ya kwanini bei ya saruji kwa kiasi hicho, Mheshimiwa Rais naanza na hilo," alisema.

Alisema: "Nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Rais nataka nianze na hilo, ilimradi wakuu wa mikoa wapo hapa nataka niwaagize na wao hadi Novemba 20, mwaka huu saa nne asubuhi kila mmoja aende palipo na kiwanda na mawakala wa saruji waangalie ni kwanini bei imependa kutoka bei ya kawaida na ongezeko la Sh. 3,000 hadi Sh. 4,000 bila sababu yoyote."

"Tukiwa tunaendelea kwenye kampeni wapo wenzetu wachache wameanza kujisahau, na tumeona kumeibuka upandaji wa bei ya saruji kwa gharama kubwa sana ambazo hazikubaliki hakuna sababu ya msingi," alisema.

Pia Waziri Mkuu alisema: "Serikali yetu katika miaka mitano iliyopita tumefanya mambo makubwa sana tumewezesha miundombinu ili kufanya biashara kwa urahisi, tumefufua hadi reli kupitia Dar es Salaam, Ruvu, Tanga, hatutarajii saruji kuwa na bei hiyo tunayoiona."

Gazeti hili Novemba 9, mwaka huu liliibua taarifa ya sakata la kupanda kwa bei ya saruji katika mikoa mbambali nchini, hali iliyosababisha wananchi kulalamika na kudai kusimamisha shughuli za ujenzi.

Bei ya bidhaa hiyo katika baadhi ya mikoa ilipanda kutoka Sh. 16,000 na 17,000 hadi Sh. 23,000 na 25,000.


ROCK CITY TAKERS LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**
**SHAURI LA MADAI 56/2017**

**PIUS MUHINDI BULENGA ........................................ MDAI**
**VS**
**SAMSON S/O PETER ........................................ MDAIWA**
**SHAURI LA MIRATHI 75/1992**

**CHARLES JOHN MAHILANE ..............................MSIMAMIZI**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA WILAYA YA SERENGETI NA MWANZO MJINI NYAMAGANA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA MDAIWA NA MAREHEMU AMBAZO NI NYUMBA SIKU YA ALHAMISI TAREHE 03/12/2020 KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA IJUMAA TAREHE 27/11/2020 KUANZIA SAA SITA MCHANA NA KUENDELEA.

MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIYOKO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA KIWANJA 525 KITALU "B" | CHAMOTO, MUGUMU - SERENGETI | SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 2 | NYUMBA PLOT NA 79 KITALU "AA" | MABATINI | SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA:**
1.MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATAILIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE,KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.

2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO:**
**0713342969/0766342969**
**0659570570/0752266026**

HABARI KITAIFA

# H/shauri zapewa majukumu usimamizi anwani za makazi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKURUGENZI Msaidizi Huduma za Posta, Caroline Kanuti, amezitaka halmashauri kufanya usimamizi na uangalizi wenye kuondoa uharibifu kwenye miradi ya miundombinu ya anwani za makazi.

Alitoa maelekezo hayo wakati akikabidhi tuzo kwa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, ambayo imeshika nafasi ya pili katika uanzishwaji wa anwani za makazi bila kutegemea fedha kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo ndiyo lenye jukumu la kuwasaidia wananchi upataji anwani hizo.

"Tuzo hizi zimetolewa kwa halmashauri mbili za mkoa wa Kagera Manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa Mkoa wa Mwanza, ambao wameonyesha nia ya kuanzisha wao wenyewe bila kutegemea fedha ya wizara," alisema Kanuti.

Kanuti alisema halmashauri ziwe na ujali wa usimamizi miradi hiyo na kuitambua kuwa ni yao, na kwamba haitakiwi kuharibiwa bali kurahisha huduma za jamii zitakazotolewa na serikali.

Alisema, mfumo huo ulianza katika mikoa ya Arusha, Dodoma, na Dar es Salaam ikitarajiwa kuenea kote nchi kwani ni sehemu ya utoaji ajira za kibiashara kwa kupeleka mizigo inayotumwa.

Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Japhet Kanoni, alisema vibao 100 vimewekwa katika barabara zilizopo ndani na nje ya manispaa hiyo.

Aidha, Kanoni alisema uwekaji wa vibao umeenda sambamba na kuweka namba katika nyumba 49 kama sehemu ya kutambua.

Aliongeza kuwa ili kuendelea na shughuli hiyo, halmashauri imetenga shilingi milioni 45 kwa mwaka 2021 kuongeza vibao 263, ili kupata jumla ya vibao 26,820.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, alisema zoezi hili litaendelea kwenye miji midogo ndani ya halmashauri za mkoa huo.

Hata hivyo, alisema mfano umeshaonyeshwa kwa Halmashauri ya Manispaa ambapo matarajio ya kufanikisha katika miji midogo yataonekana.



Vyombo vya moto vikipita kwa shida katika eneo la barabara ya Umoja wa Mataifa jijini Dar es Salaam, kujaa maji baada ya mvua kunyesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Mpango: Umaskini bado ni mkubwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAWAZIRI wawili walioteuliwa hivi karibuni na Rais Dk. John Magufuli wameahidi utumishi uliotukuka, huku wakisema kampeni zimewaonyesha uhalisia na kazi inayopaswa kufanyika katika kuwaletea Watanzania maisha bora.

Novemba 13, mwaka huu, Rais Magufuli alimteua Dk. Philip Mpango kuwa Waziri wa Fedha na Mipango na Prof. Palamagamba Kabudi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambapo wote walishikilia nyadhifa hizo kwenye Baraza la Mawaziri lililopita.

Wakizungumza jana baada ya kuapishwa Ikulu Chamwino, mawaziri hao walimshukuru Rais na washauri wake kwa kuwaamini kutumikia tena nyadhifa hizo.

**WAZIRI MPANGO**

Waziri Mpango alisema katika kampeni zake ameona umaskini bado ni mkubwa na inahitajika wafanye kazi kwa bidii kuwatumikia Watanzania.

"Ninakuahidi utendaji uliotukuka najua pamoja na kufanikiwa kuifikisha Tanzania kwenye kipato cha kati kiwango cha chini, bado huko nilipokwenda kwenye kampeni, umaskini bado ni mkubwa bado tunahitaji kufanya kazi kwa bidii kuwatumikia watu wetu fursa zipo nyingi, na inawezekana ndani ya kipindi kifupi na mimi naamini ukiwa bado umekalia kiti chako Rais, Tanzania itakuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati kwa kiwango cha juu," alisema.

Aliahidi kusimamia nidhamu ya watumishi wa wizara na taasisi zake huku akisema atashughulika na suala la uzembe, wizi na ubadhirifu wa fedha za umma kwa kipaumbele cha juu.

"Nilipokwenda kwenye kampeni, bado unaona shida kwenye miradi ya maendeleo, kuna tatizo kubwa tunaibiwa, nitakwenda kusimamia nchi nzima ili tuokoe fedha za hawa wanyonge zifanye kazi yake," alisema.

Aliongeza; "Hao wazembe maadamu umenipa kisu niseme mbele yako watupishe mapema kwa sababu huo mzigo ni mkubwa sana, huko kwingine nimesema kazi hii ni gunia la misumari, kwa hiyo watupishe tufanye kazi nchi yetu isonge mbele."

Aliahidi pia kusimamia ukusanyaji mapato ya serikali kwa ubunifu zaidi.

"Lakini pia matumizi ya serikali ni eneo ambalo bado kuna matumizi yasiyo ya tija na hili hatutaweza kuacha likaendelea...Mheshimiwa Rais nakuahidi nitabeba hotuba yako wakati wote kuhakikisha tunatekeleza ipasavyo," alisema. Kuhusu majadiliano ya sekta binafsi, alisema atajipanga upya ili awamu hii sekta binafsi ipate nafasi yake katika maendeleo ya nchi.

"Nikuhakikishie vita vya kiuchumi ni halisi na nakuahidi nitakuwa askari wako hodari katika vita hii, na muhimu sana mapato ya taifa lazima yaongezeke, suala la kwenda kuomba omba umetufundisha na mimi nachoka kuomba, inawezekana kabisa fursa zipo za kuchochea maendeleo ya Tanzania," alisema.

Aliwaomba viongozi na Watanzania kwa ajili ya vita ya kiuchumi kila mmoja ahakikishe analipa kodi ipasavyo.

"Ninawaasa watendaji wenzangu wa Mamlaka ya Mapato (TRA) mapema na maandiko yanasema tutoze kodi kama ilivyoamuriwa, tusitoze kodi kwa ziada au kuweka mfukoni," alisema. Hata hivyo, alisema alipokuwa akisoma bajeti ya serikali Juni 11, mwaka huu hakujua kama anajitwisha msalaba.

"Nilisema maneno machache kwa Watanzania, nilisema yeyote atakayeteuliwa katika nafasi ya Waziri wa Fedha moja ajinyenyekeze kwa kuwa na hofu ya Mungu, asimamie maslahi ya taifa na haki za wananchi wanyonge," alisema.

Pia alisema: "Nilisema ashinde vishawishi vya rushwa, azingatie sheria na kanuni zinazoongoza ukusanyaji wa mapato ya serikali, ukopaji wa mikopo, ugawaji rasilimali fedha na kusimamia ugawaji wa hizo rasilimali bila kuyumba, nilisema mtu huyo afuatilie mwenendo wa uchumi wa taifa na dunia na afanye hivyo kwa umakini."

"Sikua najua kwamba hiki kisu kumbe umenikabidhi mimi mwenyewe nijikate mwenyewe, nakuahidi Rais na Watanzania wote nitachapa kazi na nitayaishi haya niliyosema," alisema.

**WAZIRI KABUDI**

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliahidi kuhakikisha anakuza mahusiano ya kiuchumi na mataifa mengine, Jumuiya za Kikanda na taasisi zingine za kimataifa.

"Nakuahidi tutafanya kazi hii kwa bidii juhudi kubwa, pia tutahakikisha Balozi zetu zinakuwa kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma," alisema.

Pamoja na hayo, Prof. Kabudi alisema kimo cha msaidizi ni kifupi kwa aliyemteua na ukomo wake ni kufanya kazi aliyotumwa kwa bidii.

# EWURA, LATRA kushirikiana kuboresha usafirishaji mafuta

**Na Edwin Mhagama**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) zimeingia makubaliano ya kushirikiana katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa mafuta nchini.

Aidha, makubaliano hayo yatajikita kwenye utendaji na kuimarisha ushirikiano wa majukumu katika kusimamia sekta hiyo, kwa lengo la kujali usalama wa raia na bidhaa ya mafuta kuanzia ngazi ya uzalishaji mpaka usafirishaji wake.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, pamoja na Mkurugenzi wa LATRA, Gilliard Ngewe, kwa pamoja walisaini makubaliano hayo jana jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi EWURA, Ahmad Kilima, alisema ushirikiano huo utajikita katika kutoa elimu kwa umma na wadau wa sekta ya usafirishaji mafuta kwa ajili ya kuongeza usalama wa mazingira na kupunguza madhara yatokanayo na shughuli za usafirishaji wa bidhaa ya mafuta nchini.

"Sasa hivi utaona magari yote ya petroli, yanapita maeneo ambayo mtu hajui hatari, tutakaa kuona magari yadhibitiwe. Petrol ni kati ya bidhaa hatarishi, usafirishaji wake unahitaji umakini, tunapaswa kuwaelimisha wananchi, madereva na watumiaji," alibanisha Kilima.

Ameongeza: "Hata askari wa usalama barabarani tuwahusishe katika utekelezaji wa makubaliano haya ili wakiwa barabarani wakisimamisha gari la petroli, wajue kwamba pale wamesimamisha bomu ambalo linaweza kulipuka wakati wowote likiwa siyo salama kwa askari, madereva na wananchi waliopo katika eneo hilo."

Awali Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Ngewe, alisema makubaliano hayo yataisaidia mamlaka hiyo kukagua magari makubwa yanayobeba mafuta na kuhakikisha yanafuata taratibu za kiusalama kwa mujibu wa mamlaka zote.

Aidha, alisema mamlaka hizo hazitashindwa kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya yeyote atakayevunja sheria ikiwamo kuyaondoa barabarani magari yasiyo na sifa za kubeba mafuta.

"Kumekuwa na changamoto ya magari mabovu yanayobeba mafuta, lakini kwa kushirikiana EWURA na LATRA tutahakikisha magari yanayobeba mafuta yanastahili kuwapo barabarani, tutayaondoa barabarani," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Chibulunja, alisema mamlaka hiyo itaweza kusonga mbele kiutendaji kwa kuwa imepata usaidizi wa majukumu ambaye ni LATRA na hiyo itasaidia kuongeza ubora wa bidhaa kama mafuta kwa kuhakikisha kwamba wazalishaji na wasafirishaji wanafuata taratibu za kiusalama kabla ya bidhaa kufika kwa wananchi.

# Afungwa jela miaka 30, viboko 12 kwa kubaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Mavota, Makoye Kasindye (20), kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 12 kwa kosa la kumbaka mama mwenye umri wa miaka 28.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Kato, ulipeleka mahakamani mashahidi watatu waliothibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya ukatili kama yake.

Alisema mshtakiwa alitumia mwanya wa kutekeleza kitendo hicho baada ya mume wa mlalamikaji kukamatwa kwa kosa la kujihusisha na shughuli za uganga wa kienyeji bila kibali.

Alisema mshtakiwa alifika nyumbani kwa mlalamikaji ambaye alikuwa amelala na wadogo zake saa 6 usiku na kugonga mlango na kujifanya ni mgambo ambaye amekwenda kumchukua ili akatoe ushahidi wa mume wake.

Hakimu Maweda alisema mlalamikaji alipofungua mlango, mshtakiwa alimpiga makofi na kumvuta kwa nguvu hadi umbali wa mita 200 na kumwiingiza kwenye jengo la kanisa ambako alitekeleza unyama wake.

Alisema mlalamikaji alipiga kelele na wasamaria wema walifika na kumkuta mshtakiwa akimfanyia kitendo hicho na kumkamata na kumpeleka kwa mtendaji, hatimaye alipelekwa kituo cha polisi.

Hakimu Maweda alisema ushahidi uko wazi kwa sababu mshtakiwa huyo alikutwa anambaka mlalamikaji.

Alisema ushahidi wa kwanza na wa pili wa upande wa mashtaka unaeleza wazi kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mama huyo bila idhini yake.

Hakimu Maweda, aliukataa ushahidi wa mshtakiwa aliyeeleza kuwa alikuwa mgeni katika maeneo hayo na kwamba alikuwa anakula chakula kwenye mgahawa wa mama huyo.

Alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Alimtia mshtakiwa hatiani na alipotakiwa ajitetee, aliangua kilio huku akiiomba mahakama impunguzie adhabu kwa madai ana familia ya watoto wanne na bibi yake anayemtegemea.

Hakimu Maweda alisema baada ya kutafakari makosa ya ubakaji kukithiri katika Mkoa wa Geita na mahakama ikiwa chombo cha kurekebisha tabia, anamfunga jela miaka 30 na viboko 12, ili akajifunze tabia nzuri ya kuishi na jamii.

Awali, akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, alidai Machi 9, mwaka huu mshtakiwa alimbaka mwanamke huyo bila idhini yake kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.



Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakitoa mchanga kwenye mtaro katika eneo la Goba Njia Nne. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Tisa mbaroni tuhuma kuchoma nyumba ya diwani mteule CCM

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watuhumiwa tisa wanaodaiwa kuhusika kuchoma moto nyumba ya Diwani mteule Kata ya Kikongo (CCM), Fatuma Ngozi, na kusababisha vifo vya watu watatu siku ya tukio.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amebainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya uchunguzi wa tukio hilo kwa waandishi wa habari.

Wankyo alisema katika tukio hilo lililotokea Novemba 9 majira ya saa saba usiku katika Kijiji cha Chekeleni, Kata ya Kikongo Tarafa ya Mlandizi Halmashauri ya Kibaha Vijijini, nyumba ya marehemu diwani mteule huyo ilichomwa moto na hadi sasa watu sita kati ya saba walioku wa wamelala kwenye nyumba hiyo wamefariki dunia. Alisema baada ya tukio hilo Jeshi la Polisi limefanya uchunguzi na kuwakamata watuhumiwa tisa kati yao wanaume wanane na mwanamke mmoja, ambao wamekamatwa kutokana na taarifa na ushahidi uliokusanywa.

Kamanda Wankyo alisema watuhumiwa hao wamehojiwa wote na wanatarajia kufikishwa mahakamani.

"Kwa vile tunaendelea na upelelezi wa tukio hili, Jeshi la Polisi linaendelea kuhifadhi majina, nyadhifa na kazi za watuhumiwa kwa sababu bado tunaendelea kufuatilia na kuwakamata watuhumiwa wengine kwa kadri tutakavyokuwa tunaendelea na upelelezi wa tukio hili," alisema Wankyo.

## Shirika laibua watoto wenye ulemavu

**Na Ashton Balaigwa,** KILOSA

WATOTO 73 wenye ulemavu wa viungo wameibuliwa katika kata tisa za tarafa ya Ulaya na Magole, wilayani Kilosa mkoani Morogoro na Shirika la World Vision Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT).

Kati ya watoto hao, 47 wamepatiwa msaada wa viti mwendo.

Kuibuliwa kwa watoto hao kumetokana na Shirika la World Vision Tanzania kufanya utafiti kwenye tarafa hizo wa kubaini watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ili kumwondolea ugumu wa maisha kupitia kaulimbiu ya 'Kwa kila mtoto maisha katika ukamilifu wake'.

Akikabidhi viti hivyo, Mratibu wa Mradi wa World Vision wa Magole (AP), Wilaya ya Kilosa, Donasian Severine, alisema viti mwendo hivyo vimegharimu Sh. milioni 30.

Severine alisema, watoto wengine 74 wenye ulemavu huo wamepelekwa kufanyiwa vipimo na shughuli za kimatibabu kulingana na ushauri wa wataalamu kutoka CCBRT na baada ya hapo watapatiwa viti mwendo.

"Wastani wa watoto 26 kati ya 74 waliobuliwa, wataalamu wameshauri kwanza wakafanyiwe matibabu CCBRT kutokana na mazingira waliokuwa wakiishi baada ya hapo tutawapatia viti mwendo vyao vya kuwasaidia," alisema Severine.

"Lengo la Shirika letu ni kuangalia maeneo yenye mahitaji zaidi ili kuondoa vikwazo kwa watoto wenye mahitaji maalumu wakiwamo wenye ulemavu wa viungo hivyo tulipita kata tatu katika tarafa ya Ulaya na kata sita katika tarafa ya Magole na kuwaibua hao watoto," alisema Severine.

Mtaalamu wa mazoezi na Mratibu wa huduma za viti mwendo kutoka CCBRT, tawi la Moshi, Neophita Lukiringi, alisema utafiti wao kwa eneo la Magole na Ulaya, umebaini chanzo cha watoto wenye ulemavu wa viungo ni kinamama kujifungulia majumbani pamoja na kwa wakunga wa jadi na baadaye kushindwa kwenda kwenye zahanati na vituo vya afya kuendelea na huduma za afya ya mtoto.

Alisema kwa sasa huduma hizo zipo sehemu nyingi kutokana na kujengwa kwa zahanati na vituo vya afya vya kisasa, uboreshaji wa huduma zake na wataalamu wa aina mbalimbali wa sekta ya afya.

"Kwa sasa mjamzito anapokwenda kujifungulia katika zahanati au kituo cha afya anapatiwa msaada mkubwa pale kwa mfano mama mwenye uzazi pingamizi atasaidiwa kutokana na kuwapo kwa vifaa vya kumsaidia mtoto aweze kulia ili ubongo wake upate oksijeni mara moja," alisema Lukiringi.

# Ofisa Uhamiaji mahakamani madai ya rushwa 500,000/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imemfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, Elibarick Mnghani (29) kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 500,000.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Dodoma imefanikiwa kurejesha Sh. milion 21,276, 800 ikiwa ni madeni ya Chama cha Akiba na Mikopo (Saccos) ikiwa mkopo umiza na mapunjo baada ya kuachishwa kazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliotolewa na Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, ilisema kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ni matunda ya uchunguzi uliofanyika Novemba 13, mwaka huu.

Alisema kuwa siku hiyo majira ya usiku katika eneo la Dodoma Hoteli, mshtakiwa alishawishi kupokea rushwa hiyo kutoka kwa Saurabh Tanwar, ili asaidie kuachiwa kwa Gangeswaran Thangadurai, raia wa India ambaye alikuwa ameshikiliwa na maofisa wenzake wa Uhamiaji kwa madai ya kuwazuia kufanya kazi yao.

Aidha, Kibwengo alisema taasisi hiyo pia imemfikisha katika mahakama hiyo Hamis Athuman (27), mkazi wa jijini Dodoma, ambaye ni fundi magari wa kampuni ya Yapi Markezi na kumfungulia mashtaka ya kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 380,000 kutoka kwa watu watatu.

Alisema uchunguzi wa TAKUKURU umeonyesha kwamba kati ya Oktoba 2019, na Januari 2020, mshtakiwa alipokea fedha hizo, ili awasaidie wananchi hao kupata ajira katika kampuni anayofanyia kazi.

Akitolea ufafanuzi fedha za Saccos na mkopo umiza zilizorejeshwa, alisema kiasi cha Sh. 10,976,800 kimerejeshwa katika ofisi ya TAKUKURU wilayani Kondoa kwa uongozi wa Mkombozi Soko Kuu Saccos yakiwa ni madeni sugu ya wanachama 27.

Alisema Sh. 5,100,000 zimerejeshwa kwa askari Magereza mstaafu, Julius Mtono, baada ya TAKUKURU kuitaka kampuni ya Kihega Investment LTD, inayofanya biashara ya kukopesha fedha jijini Dodoma kurejesha fedha hizo ilizojipatia kinyume cha makubaliano baada ya kumpatia Mtono mkopo wa Sh. milioni sita Septemba 2017.

Alisema, baada ya mafao ya kustaafu Mtono kutoka Oktoba 2018, uchunguzi wa TAKUKURU umebaini kampuni hiyo ilikata fedha nyingi zaidi.

"Ukiacha huyo, pia taasisi imemwezesha Rehema Shembuli, kulipwa na aliyekuwa mwajiri wake kampuni ya Travelling -Link tawi la Dodoma mafao ya Sh. milioni 5.2 aliyostahili kupata baada ya kuachishwa kazi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Awali, kampuni hiyo haikumlipa chochote hadi alipotoa taarifa TAKUKURU baada ya kufuatilia ndipo Rehema, alilipwa kiasi hicho cha fedha.

Alisema pia wamemfikisha Mahakama ya Wilaya ya Kongwa Ofisa Afya Mkuu Msaidizi wa Mamlaka ya Mji Mdogo Kibaigwa, Anania Madoho (57), ambapo amefunguliwa mashtaka mawili ya kushawishi rushwa ya Sh. 200,000 na kupokea Sh. 160,000.

# Viongozi dini wakemea moto wa ajabu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIONGOZI wa madhehebu mbalimbali ya dini wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameungana kuombea familia tisa zilizopo eneo la kitongoji cha Hongwa Mtaa wa Shunu, Kata ya Nyahanga, ambazo hivi karibuni zilipatwa na janga la moto wa ajabu unaodaiwa kutokana na imani za kishirikina.

Aidha, viongozi hao wamewataka wananchi hao kuendelea na shughuli za uzalishaji mali kwa kuwa wamevunja ngome ya shetani aliyetawala miongoni mwao kwa maombi rasmi yaliyoongwa mkono na mwenyekiti wa mtaa huo.

Akiendesha maombi hayo Mchungaji wa Kanisa la Ukombozi Jeremiah Mussa pamoja viongozi na wenzake alisema:

"Ndugu zangu kila mmoja wetu hapa kwenye mtaa wetu afanye maombi kwa imani yake, ili kuzidi kuvunja ngome ya shetani."

"Njia pekee kila mtu anapokuwa nyumbani kwake aombe kwa imani ya dini yake japo tatizo hili linatisha na kuonekana limewashtua sana, lakini kwa kumwamini Mungu tatizo hili ni dogo sana mbele zake na Mungu yupo pamoja nanyi," alisema.

Naye Mary Mussa alisema tukio hilo siyo la kawaida kwa kuwa limewatia hofu, na kwamba jambo hilo lilianza kwenye familia ya Joseph Kioja kipindi cha Agosti 18 , 2019 na hata mwaka huu jambo hilo pia limeanza katika familia hiyo na kusambaa kwenye nyumba tisa jirani.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliwataka wananchi wa Hongwa kutoshutumiana wala kutiliana shaka kwa imani za ushirikina badala yake waangalie namna ya kuondokana na tatizo hilo.

"Ni kweli Novemba 3 mwaka huu, nilipokea taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Shunu kuwa kuna tukio la moto wa ajabu," alisema na kuongeza:

"Baada ya kujiridhisha nilibaini hasara iliyopatikana kwenye makazi tisa ya wananchi ni kuunguliwa magodoro, kwisheni na hakuna mtu aliyejeruhiwa katika ajali hiyo."

Pia Macha aliwasihi wasishutumiane, wawe wavumilivu serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa tukio hilo.

NICOL
*The Economic Shield of the Nation*

National Investments PLC
11 Serengeti Road
Mikocheni "B"
P.O. Box 7465
Dar Es Salaam

Phone: +255 22 2701436/2701348
0682 720 679
E-mail: invest@nicoltz.com
Website: www.nicoltz.com

## INTERIM DIVIDEND DECLARATION FOR THE FINANCIAL YEAR 2020

The Board of Directors of National Investments PLC is pleased to, subject to obtaining approval from the Annual General Meeting of shareholders to be held on Saturday 21st November 2020, recommend an Interim Dividend of TZS 10 per share out from the profit for the financial year 2020.

Pursuant to the dividend payment declaration, the share Register details shall remain as follows:

| | |
|---|---|
| Announcement Date | 16th November 2020 |
| Trading of Share cum Dividend | 16th November to 3rd December 2020 |
| Trading of Share Ex Dividend | 4th December 2020 onward |
| Closure of the Members Register | 8th December, 2020 |
| Dividend Payment on or by | 14th December 2020 |

Dividend will be paid directly to shareholder's bank account.

**For communication, the contact is.**
**The Registrar**
**CSD & Registry Company Limited**
**2nd Floor, NHC Corporate Office**
**Kambarage House, 6 Ufukoni Street**
**P.O Box 70081**
**Dar es Salaam**
**Mobile 0746 160 516**
**Email: registrar@csdr.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji huu kwenye zao la korosho ni fursa

**JANA** katika gazeti hili tulichapisha habari kuhusu Kampuni ya Wards Internaizomal (WHI) ya Marekani, kuonyesha nia ya kuwekeza ujenzi wa viwanda vya kisasa vya kubangua korosho.

Viwanda hivyo vitajengwa katika Manispaa ya Lindi, Mtwara na Wilaya ya Manyoni mkoni Singida, ujenzi ambao utaanza mwakani.

Tayari kampuni hiyo imeshaanza hatua za awali za makubaliano ya ushirikiano kati yake na Manispaa ya Lindi na Muungano wa wakulima wa korosho kwa vijiji vinne vinavyojishughulisha na kilimo cha korosho ambayo ni Tandangongoro, Ruaha, Chikonji na Nandambi, maarufu kama Umoja wa Wakulima wa Korosho (TARUCHINA).

Taarifa zinaeleza kuwa kiwanda kitakapoanza kazi kitabangua tani 20,000 za korosho kwa mwaka.TARYCHINA watakuwa wamiliki wakuu wa kiwanda hicho, WHI na wadau wengine watachangia fedha kwa ajili ya ujenzi wake. Inaelezwa ujenzi wa kiwanda cha Lindi utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.5 na ujenzi utaanza Juni mwakani.

Tunaona hii ni hatua kubwa katika kuimarisha kilimo cha korosho nchini, kwamba sasa wakulima watakuwa na uhakika wa mahali pa kuongeza thamani korosho yao na kupata fedha zao kwa wakati.

Kampuni hiyo imeeleza kuwa itajenga kiwanda cha kisasa Mtwara na Manyoni ambako nako kuna kilimo hicho, huku mkoani Singida ndiyo umeanza kuendeleza kilimo hicho.

Korosho ni zao kibiashara ambalo huliingizia taifa mamilioni ya fedha zikiwamo fedha za kigeni, ndiyo maana serikali imewekeza nguvu kubwa katika kilimo hicho kwa kuhakikisha wakulima wanawezeshwa.

Kuwapo kwa kiwanda cha kuongeza thamani ni hatua kubwa ambayo inatoa tumaini jipya kwa kwa wakulima ambao wakati mwingine walikosa viwanda vya kupokea korosho yao kwa ajili ya kuongeza thamani na kwenda kuuza katika soko la dunia.

Ni matarajio yetu kuwa viongozi wa serikali watatoa ushirikiano thabiti kwa wawekezaji hao ikiwamo kuondoa vikwazo vyovyote ambavyo vinaweza kukwamisha utekelezaji. Pia wananchi watapata ajira viwandani, uchumi wa eneo husika utaongezeka na serikali itapata kodi kutokana na shughuli za kiuchumi zitakazofanyika.

Uwapo wa viwanda hivi kutasaidia wakulima wasiuze korosho ghafi bali iliyoongezewa thamani, maana yake watapata kipato kikubwa kinachotokana na zao hilo.

Faida haitakuwa kwa mwananchi mmoja mmoja bali taifa kwa maana halmashauri zitapata ushuru utokanao na zao hilo, kodi kutoka kwenye viwanda na wananchi watapata ajira na kukatwa kodi, ikiwamo mzunguko wa fedha na maendeleo kwa eneo husika.

Faida ni nyingi na zinagusa kila eneo na sasa ni wakati mwafaka kwa pande zote kuhakikisha mikataba ni yenye manufaa ya pande zote na kusiwe na mkataba laghai ambao kwa namna moja au nyingine utapoteza maana ya jambo husika.


Hakuna ubishi kuwa korosho ni zao ambalo haliwezi kukosa soko wala soko lake kuyumba kwa kuwa inahitajika duniani kote na Tanzania imebarikiwa kuwa na ardhi inayostawisha zao hilo.

Ni muhimu sana kutumia neema hiyo ya Mungu kustawisha zao hilo na kuweka mifumo thabiti ya kumnufaisha mkulima na si watu wakati ambao wakati mwingine hutumia taratibu ngumu kumnyonya mkulima.

Manufaa mengine tunayotarajia ni huduma za kijamii, kwa kuwa mbali na serikali kutoa fedha, lakini wawekezaji husaidia huduma hizo, na huhakikisha wanarudisha kwa jamii sehemu ya faida.

Kwa muundo huo, manufaa ya uwapo wa viwanda hivyo ni makubwa, na sasa taifa litanufaika na uwapo wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Pacific-Astrida Kalinda

# Ombi, uongozi kitaifa uingilie kati mgogoro ardhi wenye miaka 10

**NITUMIE** nafasi hii kwa uongozi mzima wa kiserikali nchini, kuanzia kwako Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupata ridhaa ya wapiga kura wako kurejea nafasi yako katika kipindi cha miaka mitano ijayo, viongozi, wabunge na madiwani, kushika usukani wa kutuongoza kwa miaka mingine mitano inayoishia 2025.

Binafsi nianze kwa kujitambulisha kwamba ni Mtanzania kwa sasa ni mkazi wa Tegeta, jijini Dar es Salaam. Naomba niwasilishe kero yangu binafsi ambayo sasa inanisumbua kwa miaka 10 pasipo majibu sahihi.

Nimeamua nitumie njia ya waraka huu kutafuta msaada na ikiwezekana ofisi yako kuu kitaifa, inisaidie kutatua suala hilo lishe.

Kimsingi, huko nyuma mwaka 2007, niliomba na kupewa viwanja vyenye namba: 3016, 3017, 3018 na 3019 vilivyoko Burega, katika Halmashauri ya Mji wa Ujiji/Kigoma, lengo ni kujenga hoteli pembezoni mwa Ziwa Tanganyika.

Mwaka 2010 nilianza kazi hiyo kwa kujenga uzio, ambao ghafla katika hali ya kushangaza niliona imevamiwa na kubomolewa na waliodai kuwa hapo ni mali yao.

Niliripoti suala hilo kwa mamlaka zinazohusika, kabla ya wavamizi hao kuanza kujenga nyumba. Ripoti hiyo niliipeleka kwenye Halmashauri ya Mji wa Kigoma na barua nyingine nilipeleka katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilipokuwa makao makuu jijini Dar es Salaam, kwa hiyo waliingilie kati hilo.

Sikukaa kimya, bali niliendeleza ufuatiliaji katika ofisi zote mbili pasipo mafanikio ya maendeleo chanya ya aina yoyote ile. Kuna wakati niliitwa na nikahojiwa mengi, kisha nikaahidiwa majibu. Hapo kukatawala kimya kikuu kisicho na majibu hadi sasa.

Nitamke hadi naandika barua hii, mahali hapo kuna watu wanaendelea kujenga nyumba. Mara ya mwisho kulipia kodi ya makazi ilikuwa mwaka 2012, ndipo nilipojulishwa na wahusika wa Idara ya Ardhi, walionitaka niache kulipa kodi hiyo, mpaka mgogoro utakapomalizika.

Leo hii ninapoandika barua, nimeshahudhuria wito mara mbili huko Kigoma, ambako niliwasilisha nyaraka zangu na mpaka sana hakuna ushuhuda wa suluhisho la aina yoyote ile.

Mara ya mwisho kwenye kikao, niliulizia kama niwakilishe suala hili mahakamani na ikiwa ni hivyo, je, nimshitaki nani? Nilijibiwa 'nisubiri kidogo' na imefika hadi leo hakuna suluhu inayoonekana wala ufafanuzi unaoipa mwanga wa kinachoendelea.

Binafsi, nimekwishaangaika katika ofisi mbalimbali zinazohusika kwa muda wote huo, nimebaki kizani hatima ya mgogoro huu ni nini au njia inayofuata?

Waliokuwapo muda huu wote kwenye nafasi za Halmashauri na Ofisi ya Ardhi walishughulikia hilo, wameshaondoka kwa sababu mbalimbali. Hivyo, kila ninapofuatilia jambo hili linakuwa jipya na ninaambiwa nipeleke upya karatasi zote zinazohusika. Kwa hali hii nimechoka, kwa sababu gharama inakuwa kubwa mno katika msuguano usio na majibu.

Najua ingawa sasa wizara inayohusika na ardhi bado haijawa na waziri, lakini safu ya uongozi kuanzia mtendaji wake mkuu kwa maana ya Katibu Mkuu na timu ya makamishna, pia wakurugenzi na maofisa wengine wa chini yao.

Vivyo hivyo niseme, hata katika ngazi ya Halmashauri ya Mji Ujiji/ Kigoma kuna safu ya kitaalamu ambayo kimsingi katika mfumo ulioko sasa, Idara ya Ardhi inawajibika moja kwa moja na wizara mama.

Mbele ya Rais wetu na timu yake ya uwajibikaji, naomba ifike hatua suala hili likafikia mwisho maana liko ndani ya utendaji wa kiserikali.

Pia, niko katika faraja pale niliposhuhudia kuteuliwa na kuapishwa Mtendaji Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, nikifahamu kasi yake katika kutoa msukumo unaozaa majibu kwa shida zinazowakwaza wananchi.

Niweke wazi msimamo wangu muda wote, kwamba sipendi kulihamishia hili mahakamani, hivyo naomba uamuzi wowote utakaotolewa kiserikali, binafsi nitauheshimu. Napatikana kwa simu namba 0713 242216, kwa yeyote anayehitaji kupata ufafanuzi nimpe ushirikano, nikiwa na nyaraka zote muhimu zitakapohitajika.

## HABARI KITAIFA



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, Fatuma Mapunda, alipokuwa katika mjumuiko wa elimu unaohusu mageuzi na mwamko wa kijinsia na maendeleo juzi, ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). **PICHA: SABATO KASIKA**.

# Wajadili athari za corona kwa wajasiriamali wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

KINAMAMA wajasiriamali wamekutana katika kongamano la 'Woman of Influence, I'm Possible' kujadili vikwazo vilivyotokana na ugonjwa wa Covid-19 nchini kwenye shughuli zao.

Pia walijadiliana namna ya kujikwamua na vikwazo hivyo katika kongamano hilo lililoratibiwa na Mkurugenzi wa The East Africa Bang! Magazine, Emelda Mwamanga, na kufanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wanawake wajasiriamali na wageni mbalimbali, ambapo mijadala na mada anuai ziliwasilishwa kuwajengea uwezo kinamama hao.

Akizungumza na wanahabari katika kongamano hilo, Mwamanga alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha kinamama na kujadili changamoto zilizojitokeza, kushirikishana namna ya kukabiliana nazo na kuwajengea uwezo jamii hiyo kufanya vizuri zaidi kwenye shughuli zao kwa mwaka ujao.

Alisema sehemu kubwa ya biashara zikiwamo za kinamama ziliathirika kiasi kikubwa na ujio wa janga la corona, hivyo kuna kila sababu ya kuyajengea uwezo makundi mbalimbali wakiwamo kinamama wajasiriamali kukabiliana na janga hilo.

Naye Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Kampuni ya ZARA Tours, Zainab Ansell, akizungumza kwenye kongamano hilo, alisema wajasiriamali wanawake waliopo katika sekta ya utalii wamejipanga kuhamasisha utalii wa ndani ili kuziba pengo la upungufu wa watalii kutoka nje lililotokana na janga la corona.

Alisema Tanzania ina sehemu nzuri na za kujivunia za utalii, hivyo Watanzania wanatakiwa kuelimishwa na kuhamasishwa kuzitembelea.

# Kaya 1,260 zanufaika elimu ya kilimo hai

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya kaya 1,260 za tarafa saba za wilaya za Gairo na Kilosa mkoani Morogoro zimeanza kunufaika na elimu ya kilimo hai cha mahindi.

Kaya hizo zimeinuka kutoka kuvuna debe nne hadi sita kwa shamba la hekari moja hadi kufikia kuvuna gunia 10 hadi 15 za mahindi na kuwa na uhakika wa chakula kwenye kaya tofauti na hapo mwanzo.

Ofisa Kilimo wa mradi wa mpango wa maendeleo jumuishi wa jamii (ICDP), Emmanuel Kasembe, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa utekelezaji wa mradi huo unafanyika chini ya ufadhili wa Shirika la misaada la Ujerumani kupitia Kanisa la Anglikana Tanzania - Dayosisi ya Morogoro.

Alisema wakulima hao kutoka vijiji 14 vya tarafa saba kwenye wilaya za Kilosa na Gairo watazidi kunufaika na kilimo cha mahindi na mazao mbalimbali yakiwamo mboga na matunda ambapo alizitaja tarafa hizo ni Maguha, Mtumbatu, Iyogwe, Italagwe, Lubeho na Nongwe.

Alisema kabla ya mradi huo walifanya utafiti na kubaini kuwa kaya moja yenye watu 4 hadi 6 ilikuwa na uwezo wa kuzalisha debe 4-6 za mahindi ambazo ni sawa na kilo 400 -600 kutokana na upandaji usiozingatia kanuni za kilimo licha ya kulima eneo kubwa.

Alisema kwa kawaida kaya au familia ya watu 4-6 hutakiwa kuwa na uhakika wa gunia 5- 6 za mahindi ambapo baada ya wakulima hao kuingia mkataba wa makubaliano ya kilimo hicho wameanza kuona manufaa hayo na kuendelea kulima kwa kufuata kanuni walizoambiwa ili kuboresha kilimo.

Aliwaomba wadau wa kilimo kuiga elimu wanayotoa kwenye tarafa za wilaya hiyo ili kuinua wakulima wengi nchini ambao hutumia eneo kubwa na kupata mazao kidogo.

Naye Mratibu wa mradi, Stella Sabuhoro, alisema mradi huo wa miaka mitatu ulianzishwa mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2022 katika wilaya hizo za Kilosa na Gairo ambao uliwapeleka baadhi ya wakulima hao eneo la Chinangali jijini Dodoma, Zanzibar na Morogoro na kupata mafunzo ya namna ya kushirikiana na kuwasiliana na wakulima wengine kimasoko.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU WAAJIRIWA KUWA NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) KABLA YA TAREHE 31 DISEMBA, 2020

Ikumbukwe kwamba mnamo tarehe **6 Agosti 2020,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilizindua mfumo wa uwasilishaji ritani za kodi kwa njia ya mtandao **(e-Filing)** ambapo, pamoja na ritani zingine, mfumo huu unajumuisha ritani ya zuio katika mapato ya waajiriwa, yaani, Pay As You Earn (PAYE).

Kutokana na mabadiliko hayo kuanzia sasa kila mwajiri atalazimika kuwasilisha ritani ya zuio katika mapato ya waajiriwa (PAYE) ikionesha namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) ya kila mwajiriwa na kodi husika iliyokatwa.

Kwa waajiriwa ambao TIN tayari wanazo, mwajiri ataziingiza katika ritani zake kuonesha kiasi cha kodi kilichokatwa kwa mwajiriwa husika na kuwasilishwa TRA.

Aidha, kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, na kwamba ama wana Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) au Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN), wanaelekezwa kuomba TIN hizo kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa **Online TIN Registration** unaopatikana kwenye tovuti ya TRA (ambao ni **www.tra.go.tz**). Kwa waajiriwa wasio na Kitambulisho cha Taifa watalazimika kutembelea Ofisi za TRA kupigwa picha na kuchukuliwa alama zavidole.

Hata hivyo, waajiri wanaelekezwa kuwa kwa waajiriwa ambao kwa sasa hawana TIN, waajiri wataingiza namba ya TIN ya mfano ambayo ni **999 999 999** wakati wa kuwasilisha ritani za kodi ya ajira kwa ajili ya kuwezesha kushughulikia mishahara yao.

Vile vile, tunapenda kutaarifu kwamba ukomo wa utaratibu huu kwa wasio na TIN ni hadi mnamo **tarehe 31 Desemba 2020.** Baada ya hapo hakutokuwa na muda wa nyongeza. Hivyo, tunawaomba na kuwasihi waajiri na waajiriwa wote wajitahidi kutekeleza wajibu wao katika muda uliowekwa hasa ikizingatiwa kuwa mlipakodi anapaswa kuwa na TIN ikiwa ni matakwa ya **Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 R.E 2019.**

Kwa maelezo zaidi; unaweza kutembelea Ofisi ya Mamlaka iliyo karibu nawe. Pia, unaweza kutembelea tovuti ya TRA (**www.tra.go.tz**) au kupiga simu bure kupitia **0800 750 075** au **0800 780 078,** na kutuma ujumbe wa WhatsApp (0744 23 33 33) au kutuandikia barua pepe kwa anwani pepe **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz**.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na;**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI TRA MAKAO MAKUU**

# Mil. 830/- zakopesha wajasiriamali Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya Sh. 830,442,000 zimetolewa mikopo kwa wajasiriamali kisiwani Pemba kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka huu.

Kati ya fedha hizo, Wilaya ya Wete zilitolewa shilingi 225, 400,000 kwa mikopo 281, Wilaya ya Chakechake Sh. 273,000,000 kwa mikopo 289. Wilaya ya Mkoani ilipata shilingi 180,042,000 kwa mikopo 233 na Wilaya ya Micheweni shilingi 152,000,000 kwa mikopo 181.

Akizungumza na Nipashe Gombani Chakechake, Mratibu wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Pemba, Haji Khamis Haji, alisema jumla ya mikopo 984 imetolewa kwa vikundi na mtu mmoja mmoja.

Alisema kuwa, kati ya fedha hizo zilizotolewa mikopo, jumla ya shilingi 606,456,800.00 zimesharejeshwa, ambapo Wilaya ya Wete ni shilingi 156,613,000.00, Chakechake shilingi 192,114,000.00, Mkoani shilingi 136,818,500.00 na Micheweni shilingi 120,911,300.00.

Alisema lengo la kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapa mkopo ni kuwaongezea mitaji, ili wazalishe zaidi na wapate mafanikio.

"Kabla ya kuwapa mikopo tunawapa mafunzo, ili wajue namna ya kutumia kwa lengo waliloombea na sio vinginevyo, ili wasiende kinyume," alisema mratibu huyo.

Mratibu huyo aliwataka wajasiriamali kuanzisha miradi inayozalisha zaidi na kuleta tija, jambo ambalo litawasaidia kuingiza kipato kitakachowakwamua na maisha duni.

"Ili tumpe mkopo ahakikishe ameanzisha mradi ambao unaleta maendeleo na upo hai na awe na kikundi amekisajili benki, hivyo mtaji tutakaompa utamsogeza mbele katika harakati zake za ujasiriamali," alifafanua.

Naye mjasiriamali wa ushonaji wa mikoba ya ukili, Time Khamis Mwinyi mkazi wa Micheweni, alisema alipata mkopo mwaka jana na anaendelea kulipa kama alivyopangiwa.

# Wanakijiji waokota miili iliyotelekezwa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MIILI ya watu wawili wanaume wanaokadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 20 hadi 25, imeokotwa katika eneo la kijiji cha Mkowela katika kata ya Namakambale wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

Inadaiwa kuwa miili hiyo ilitelekezwa na watu wasiojulikana na kuzua hofu miongoni mwa jamii.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema kuwa wakazi wote wa kijiji hicho, walishindwa kuitambua, hivyo walitoa taarifa polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Baada ya kuripotiwa taarifa hizo, Jeshi la Polisi liliichukua miili hiyo na kwenda kuihifadhi kwenye chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali ya serikali ya wilaya hiyo kwa uchunguzi zaidi.

Akizungumzia tukio hilo, Diwani mteule wa Kata ya Namakambale, Mfaume Wadali, alisema kuwa miili



hiyo iligunduliwa Novemba 14, mwaka huu na kijana wa kifugaji ambaye ilidaiwa walipita katika eneo hilo akiwa anaokota embe.

Wadali alisema kuwa baada ya tukio hilo kijana huyo aliende kutoa taarifa kijijini ambapo yeye, viongozi wa kijiji na baadhi ya wazee maarufu waliendа katika eneo la tukio na kukuta mwili wa kwanza ukiwa umelala, huku sura yake ikiwa imetazama chini na walipotazama umbali wa kama mita 100 waliona mtu mwingine akiwa amelala pembeni ya barabara na walipokwenda pia kumtazama walimkuta akiwa amekufa.

Alisema walitoa taarifa kituo kidogo cha Polisi Nakapanya na baadaye wakasambaza taarifa hiyo, katika vijiji vilivyopo jirani na eneo hilo ambapo wananchi wengi walijitokeza kwenda kuwatambua, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyeonyesha kuwafahamu, hivyo polisi kuichukua na kuipeleka hospitali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa (pichani), alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kwamba Polisi wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo chake.

Aidha, amewataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Tunduru ambao wamepotelewa na ndugu zao kwenda katika hospitali ya serikali ya wilaya hiyo, ili kuwatambua na kuwasaidia polisi kubaini ukweli wa tukio hilo haraka.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

SALAMU ZA PONGEZI





Kamati ya Taifa ya Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF, inakupongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** na Makamu wa Rais **Mhe. Samia Suluhu Hassan** kwa ushindi mkubwa mlioupata katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Ushindi huo ni kielelezo thabiti cha imani kubwa walionayo Watanzania kwenu. TASAF inaahidi kuendeleza falsafa ya Serikali yako ya "Hapa Kazi Tu" kwa vitendo kupitia utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF.

Mkurugenzi Mtendaji
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF
S.L.P 2719 Dodoma, Tanzania
Simu: + 255 26 296 3866, Nukushi: + 255 26 296 3871
Tovuti: **www.tasaf.go.tz** Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**

# Wakulima mahindi, mpunga wapatiwa mbolea bora zaidi

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WAKULIMA wadogo wa mahindi na mpunga wamewezeshwa baada ya kuzinduliwa kwa mbole mpya ambayo itawapatia mavuno mengi zaidi.

Uwezeshaji huo umefanywa na Kampuni ya YARA Tanzania ambayo ni mzalishaji na muuzaji mkubwa wa mbolea nchini, ambayo imezindua bidhaa mpya sokoni inayojulikana kama "MiCROP", ili kusaidia wakulima hao wadogo kupata mavuno zaidi.

Akizindua bidhaa hiyo mpya wilayani Kasulu mkoani Kigoma mwishoni mwa wiki mbele ya wanahabari, wakulima, maofisa wa serikali na wasambazaji, Meneja Biashara wa YARA Tanzania, Philipo Mwakipesile, alisema MiCROP ni mbolea ya kipekee kuzalishwa nchni.

Mwakipesile alisema mbolea hiyo mpya ni ya kwanza kuchakatwa Tanzania na kampuni ya YARA, ambayo itawasaidia wakulima wadogo kwani inavirutubisho vya Zinc na Sulphur Micronutrients zinahitajika kwa mazao yaweze kuwa na viwango na bora.

"Tunajivunia kuzindua mbolea ya MiCROP hapa mkoani Kigoma, ambapo wakulima wadogo wa mahindi na mpunga watapata fursa ya kuongeza mavuno sambamba na kuongeza mapato zaidi na chakula," alisema.

Mwakipesile aliongeza kuwa mbolea hiyo itachakatwa kwenye kiwanda cha YARA kilichopo jijini Dar es Salaam na hivyo kuwa mbolea ya kwanza Yara Tanzania kuchakatwa hapa Tanzania.

"Kama YARA Tanzania tunatekeleza azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025 kwa kuzalisha bidhaa hapa nchini," alisema meneja huyo na kuwataka wakulima kuchangamkia bidhaa hiyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Kasulu, Masalo Aron, alisema uzinduzi huo mjini Kasulu ulifuatia ombi la wakulima wenyewe kutaka uzinduzi ufanyike wilayani humo.

"Ni mategemeo yetu kuwa msimu ujao wa mavuno wakulima wa mahindi na mpunga mkoani hapa watajiweka katika nafasi nzuri. Wakulima wana imani kubwa na bidhaa yenu," alisema.

Wakati wa hafla hiyo ya uzinduzi, timu kutoka YARA Tanzania ilikabidhi bidhaa hiyo mpya kwa wasambazaji wao na kuonyesha sampuli ya bidhaa kwa wote waliohudhuria.

**Ni mategemeo yetu kuwa msimu ujao wa mavuno wakulima wa mahindi na mpunga mkoani hapa watajiweka katika nafasi nzuri. Wakulima wana imani kubwa na bidhaa yenu**

# Bahi wanufaika na elimu ya uzazi salama, ukatili

**Na Yasmine Protace, aliyekuwa** DODOMA

MRADI wa Tutimize Ahadi, umezaa matunda katika vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, ambapo jamii imepatiwa elimu ya uzazi salama ikiwamo na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

Awali kabla ya jamii haijapatiwa mradi huo, matukio ya ukatili yalikuwapo ambapo, wajane walirithiwa, wanawake hawakuweza kushiriki katika maamuzi, kupata vipigo na vijana wa kiume walikuwa wakijua masuala ya uzazi yanawahusu wanawake pekee.

Hayo yalisemwa na Mtendaji Kata ya Lamaiti, Yunus Magembe, wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya mafanikio ya mradi wa Tutimize Ahadi unaofadhiliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Restless Development.

"Kabla ya mradi kuwapo, matukio yalikuwapo katika kata hii ya Lamaiti, ambapo jamii ilikuwa haijui haki zao na kujikuta wakifanyiwa ukatili," alisema.

Aliongeza kuwa awali kulikuwa na ukatili wa kipigo, wajane kurithiwa, wanawake kutoshirikishwa katika maamuzi.

Alisema baadha ya kuanzishwa kwa mradi na kutolewa elimu, sasa wajane wameanza kujitambua katika kuzijua haki zao, pia vijana wa kike na kiume wameanza kushiriki katika vituo vya afya na kupatiwa elimu ya masuala ya uzazi salama.

Alisema mradi huo umesaidia kupunguza matukio ya kikatili, ambapo kamati zenye wajumbe zimeanzishwa, pia ameteuliwa mwenyekiti wa migogoro ya jamii.

Polisi kata, wameteuliwa watu mashuhuri wa kike na wa kiume na viongozi wa dini wasiopungua 18.

Alisema lengo kubwa ni kukutana na makundi hayo katika vikao na kuendelea kuzungumzia masuala ya ukatili.




Mwenyekiti wa Soko la Kambarage Manispaa ya Shinyanga, Seif Mtete, akielezea hali ya usafi wa mazingira sokoni hapo jana. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# Walalamikia funza sokoni kwenye mitaro ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Kambarage Manispaa ya Shinyanga ambao wanauza bidhaa zao pembezoni na mitaro ya kutiririsha maji, wamelalamikia kuwapo na funza kwenye mitaro hiyo, kitendo ambacho kinatishia usalama wa afya zao na wateja, kwa kupatwa na magonjwa ya mlipuko.

Wamesema mitaro hiyo kwa mbele imeziba, ambapo maji machafu yanapotoka juu hufika mahali hutuama jirani na biashara zao, huku yakiwa na funza wadogo, na kuendelea kufanya biashara hivyo hivyo licha ya kujua ni hatari kwa afya zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Jaffari Mzee, ambaye anauza bidhaa za ndizi pembezoni na mtaro wa kutiririsha maji, alibainisha hayo jana wakati Nipashe ilipotembelea sokoni hapo ili kujionea hali ya usafi wa mazingira.

Alisema wafanyabiashara ambao wanauza bidhaa zao jirani na mitaro ya kutiririsha maji, wapo katika hatari kubwa ya kupatwa na magonjwa ya mlipuko, kutokana na mitaro hiyo kuziba na kusababisha maji kutuama, huku yakiwa na funza ndani yake.

"Ndugu mwandishi wa habari kama unavyojionea mwenyewe, hapa kwenye mtaro wa maji ndani yake kuna funza, na bidhaa zetu zipo hapa pembeni... hii ni hatari sana katika afya zetu na wateja pia, tunaiomba serikali ituzibulie mitaro hii, ili maji yasikae hapa ili kuzuia magonjwa ya mlipuko," alisema Mzee.

Mwenyekiti wa Soko la Kambarage, Seif Mtete, alisema suala la usafi wa mazingira sokoni hapo wanajitahidi kulizingatia, isipokuwa tatizo la mitaro ya kutiririsha maji kuziba, pamoja na baadhi ya maeneo kutuama maji, na kubainisha kuwa wameshaliwasilisha kwenye uongozi husika wa manispaa.

Aidha, alisema katika kipindi hiki cha msimu wa mvua, suala la usafi wa mazingira kwenye masoko ni la muhimu sana, na kuiomba serikali ijitahidi kuyashughulikia kwa haraka maombi ambayo wanayawasilisha kwao, ili yapate utatuzi na kudhibiti tatizo la mlipuko wa magonjwa kikiwamo kipindupindu.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Kuchibanda Snatus, alisema wanatarajia kufanya ukaguzi wa usafi kwenye masoko yote, na kubainisha kuwa suala la kuzibua mitaro na kuweka vifusi kwenye maeneo yanapotwama maji watalifanyia kazi.

HABARI KITAIFA

## Ulaji vyakula vyenye lishe bora wahimizwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

JAMII wilayani Masasi mkoani Mtwara, imeshauriwa kuepuka kula vyakula visivyoendana na lishe bora kwa afya zao.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia kupunguza kasi ya magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka mitano.

Ushauri huo ulitolewa jana wilayani Masasi na ofisa lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Victoria Ngatunga, alipokuwa akitoa taarifa ya lishe ya robo ya mwaka wa fedha 2020/2021 kwenye kikao cha kamati ya lishe kilichohudhuriwa na wajumbe wa kamati hiyo ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Alisema kumekuwa na tatizo kubwa kwa jamii kukosa elimu kuhusu ulaji wa aina ya vyakula ambavyo vinaweza kujenga afya bora, hivyo jamii kujikuta ikikabiliwa na magonjwa mbalimbali ikiwamo kisukari, shinikizo la damu pamoja na upungufu wa damu kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

Ngatunga alisema moja ya sababu kubwa inayochagia kuwapo kwa magonjwa hayo ni pamoja na jamii kujijengea utamaduni wa kupenda kula vyakula vya aina moja kila siku hususan vya wanga.

Alisema hali ya ulaji wa vyakula ambavyo si rafiki kwa afya inapelekea mwili kukosa baadhi ya virutubisho na kukosa lishe bora kiafya.

Alisema ulaji wa vyakula vya aina moja kila siku na kupenda kula vyakula vyenye kiwango kikubwa cha mafuta pamoja na vyakula vilivyokobolewa ni miongoni mwa sababu pekee inayochangia kuwapo kwa magonjwa hayo katika jamii.

"Tupende kula vyakula vinavyojenga afya zetu ikiwamo kula mboga za majani na matunda kwani vinasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha lishe bora mwilini pamoja na kuwa na kinga imara ya mwili itayoweza kukabiliana na magonjwa mbalimbali," alisema Ngatunga.

Alisema magonjwa mengine ambayo yamekuwa ni tatizo kutokana na ulaji usiongatia lishe bora ni pamoja na utapiamlo mkali kwa watoto, hivyo elimu ya ulaji bora wa vyakula lazima itolewe kwa jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Changwa Mkwazu, alisisitiza jamii kuzingatia ulaji bora wa vyakula vyenye lishe.

Aidha, alimtaka ofisa lishe huyo wa halmashauri hiyo ya wilaya kuwa na programu ya kupita maeneo mbalimbali kutoa elimu kwa jamii ili kuwajengea watu uwelewa kuhusu lishe na afya.

# TBA kuendelea kuokoa fedha za serikali

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAKALA wa Majengo (TBA), umesema utaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ya serikali mkoani Mwanza, ili kuokoa fedha nyingi ambazo zingepotea kwa makandarasi binafsi.

Akizungumza na Nipashe jijini Mwanza, Kaimu Meneja wa TBA Kanda ya Ziwa, Moses Urio, alisema miradi waliyopewa na serikali wameisimamia na baadhi imekamilika na mingine ipo hatua za mwisho kukamilika.

Alitaja baadhi ya miradi waliyopewa na serikali Kanda ya Ziwa kuwa ni upanuzi wa Hospitali ya Serikali ya Sekou Toure, jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana na makazi ya mkuu wa mkoa.

Alisema TBA inafanya kazi katika wilaya zote za Mkoa wa Mwanza, na kwamba kwa kutumia wataalamu wake na binafsi wanafanya kazi hizo kwa gharama nafuu ikilinganishwa na kampuni binafsi za ujenzi.

Kuhusu upangishaji wa nyumba zao zaidi ya 600 zilizopo Kanda ya Ziwa, Urio alisema, wanakabiliwa na changamoto ya wapangaji kushindwa kulipa kodi kwa wakati.

Urio alisema wapangaji wengi wanashindwa kulipa kodi licha ya kuwa ni nafuu pamoja na baadhi yao kupangisha watu wengine wanapotaka kuondoka kwenye nyumba hizo.

"Nyumba zetu zimeenea mkoa wote wa Mwanza pamoja na wilaya zake na wapangaji wanaoshindwa kulipa tunatumia madalali wa mahakama kuwaondoa na kuweka watu wengine," alisema.

Aliongeza kuwa utaratibu wao unakataza mtu kupangisha ama kumrithisha mtu ama ndugu, na kwamba kila baada ya muda huwasaka watu wa namna hiyo.

Meneja huyo alisema watu wanaobainika kukiuka utaratibu wa kupangishwa nyumba hizo, huondolewa kinguvu na kuwapa wapangaji wengine waliofuata taratibu.



Wakazi wa Malamba Mawili, jijini Dar es Salaam, wakivuka jana kwenye daraja la kienyeji lililotengenezwa na baadhi ya wakazi wa eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Hospitali Bugando ilivyofanya upasuaji mkubwa wa kwanza

**Na Richard Makore,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Bugando jijini Mwanza, imefanikiwa kufanya upasuaji mkubwa kwa mara ya kwanza kwa kutoa nje utumbo mpana wa mgonjwa.

Hayo yalibainishwa juzi na Daktari Bingwa wa upasuaji wa hospitali hiyo, Dk. Vihar Kotecha, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza.

Dk. Kotecha alisema upasuaji huo ulifanyika kwa mafanikio makubwa kwa kushirikiana na madaktari wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afya cha Bugando.

Alisema upasuaji huo umefanyika kwa mafanikio makubwa, na kwamba mgonjwa huyo sasa atatumia utumbo mwembamba pekee maisha yake yote.

Aliongeza kuwa kwa sasa mgonjwa huyo ametobolewa sehemu ya tumbo lake, ili kutoa haja kubwa, na kwamba hali yake inaendelea vizuri.

Daktari huyo aliongeza kuwa utoaji nje utumbo haikuwa kazi rahisi, lakini kutokana na utaalamu waliweza kufanikisha.

Kutokana na hatua hiyo, mgonjwa huyo atalazimika kutumia utumbo mwembamba ambao utafanya kazi kama ilivyokuwa inafanywa na utumbo mpana.

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 17, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## Richter amegundua kipimo cha tetemeko, kinapunguza maafa

Ukurasa 14





Ukurasa 13

**CHAWATA inavyoibua dozi kutiba matatizo ya watu wenye ulemavu**



Ukurasa 12

Ni vipi elimu leo inaakisi uhalisia katika karne ya 21?

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Mahakama Kuu inavyokuhimiza usiache kuandika wosia

BAADHI ya familia huanza kugombea mali za ndugu zao marehemu na mzozo huwa mkubwa na mgumu kuutatua hasa pale inapotokea aliyefariki ana utajiri mkubwa na hakuacha wosia.

Vilevile, hata kama kuna wosia, bado inaibuka migogoro katika mahakama za mwanzo na hata zile za juu, inayompinga msimamizi kwa tuhuma za kufuja mirathi.

Wakati mwingine mashauri ambayo hufunguliwa na ndugu wa marehemu, kutokana na uteuzi mbaya wa msimamizi wa mirathi hali inayoweza kuleta madhara makubwa kwenye familia.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Devotha Kamuzora, anawakumbusha Watanzania kuzingatia elimu inayotolewa mara kwa mara kuhusu uandishi wa wosia na uteuzi wa wasimamizi waaminifu wa mirathi.

Akizungumza kwenye semina ya mirathi na wosia iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kuhusisha wadau mbalimbali nawashirika.

Anafafanua kuwa, wosia ni kauli au maandishi anayotoa mtu kuhusu namna angependa mali yake igawanywe iwapo atafariki. Zipo aina mbili za wosia ambazo ni maandishi na kauli.



Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Dovetha Kamuzora, akizungumzia umuhimu wa uandishi wa wosia. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### MIRATHI NI NINI?

Anasema, mirathi ni utaratibu unaotumika kusimamia kisheria mali za marehemu na haki za warithi na imejikita zaidi kwenye kuangalia ni namna gani wategemezi au ndugu waliowaacha wamuenzi ama watasimamia mali na malengo yake aliyoyapanga kabla ya kufa.

"Kwa sababu hiyo, ni muhimu kufahamu juu ya uendeshaji wa mashauri ya mirathi, kwani kwa mujibu wa kanuni ya 2 nyongeza ya 5 ya Sheria ya Mahakimu ya 2002, shauri la mirathi huanza pale ambapo mahakama kupitia maombi ya mtu yeyote inapokea maombi ya kumteua yeyote kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu," anasema Kamuzora.

Anasema, katika mahakama za wilaya na mahakama kuu, maombi hufanywa kwa kuwasilisha kimaandishi kwa mujibu wa sheria.

"Maombi yanaweza kuwa ya kuomba kuteuliwa kusimamia na kutekeleza wosia wa marehemu kwa yule aliyeacha wosia ama kuomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ambaye hakuacha wosia," anasema Kamuzora.

Anasema, mahakama za mwanzo zimepewa mamlaka ya kusikiliza mashauri yote ya mirathi endapo sheria husika ni ile ya kimila ama kiislamu na kigezo muhimu kwa mahakama zote ni kuwa marehemu wakati wa kifo chake alikuwa na makazi kwenye eneo lililoko ndani ya mamlaka ya mahakama husika.

"Ili mtu aweze kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi, mahakama haina budi kujiridhisha kuwa mtu huyo ana akili timamu, ni mwaminifu na ana uwezo wa kukusanya na kutunza hesabu za mali za marehemu," anasema.

### UMUHIMU WA WOSIA

Wosia ulioandikwa kisheria, unaweza kuepusha migogoro baina ya warithi na kuwa kauli au maandishi hayo ndiyo maamuzi ya mwisho katika kugawa mali ya marehemu, anasema Kamuzora.

"Mtu aliyetimiza umri uliokubalika kisheria wa miaka 21 na mwenye akili timamu anayeweza kuandika wosia na kuongeza kuwa unaweza kukataliwa iwapo itagundulika kuwa mwandishi alikuwa na kichaa au mlevi," anasema Kamuzora.

### UTARATIBU MAANDILIZI

Anasema wosia wa kauli na si maandishi unapaswa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopungua wanne.

"Wawili kati yao wawe ndugu wa karibu na mtoa wosia na wengine wawili wanaweza kuwa watu baki, lakini wosia huu hautafatwa iwapo mashahidi wote wamefariki kabla ya mtoa wosia na iwapo wamebaki wawili kati yao basi utafatwa," anasema Kamuzora.

Kwa upande wa wosia wa maandishi anakumbusha kuwa unapaswa kutolewa mbele ya mashahidi wasiopungua wawili, mmoja kutoka katika ukoo au familia na mwingine asiye mwanafamilia na uandikwe kwa kalamu ya wino na si penseli.

Anasema, mashahidi wajue kusoma na kuandika na wosia uwe na tarehe, sahihi ya mtoa wosia na kama hajui kusoma na kuandika, ataweka sahihi ya dole gumba la mkono wa kulia ukithibitisha jina la msimamizi wa mirathi.

"Wosia wa maandishi haubadilishwi na wa kauli ila wa kauli unaweza kubadilishwa na wa maandishi, mtoa wosia ana haki ya kuandika ama kutaja sehemu ya mali zake lakini ambazo hazijaandikwa zitasimamiwa kwa utaratibu wa mirathi," anasema.

### MSIMAMIZI MIRATHI

Anasema, yeyote anayeomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi, hana budi kufika mahakamani kuomba ateuliwe na anapaswa kuwasilisha mahakamani hati ya kifo cha marehemu na mukhtasari wa kikao cha ndugu wa marehemu kama upo.

"Kwa upande wa mahakama za mwanzo, mwombaji anapofika mahakamani anapaswa kujieleza mahakamani kwa kujaza fomu namba moja kwa usahihi taarifa za tarehe ya kifo na mahali kilipotokea," anasema.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ni vipi elimu leo inaakisi uhalisia katika karne ya 21?



Elimu ikilenga kuwapa wanajamii maarifa ni mwanzo wa kumudu maisha yao, lakini ikibakia ya kukariri kanuni za hesabati kama 'pai' huwa kitendawili kinachotakiwa kupata jawabu. **PICHA MTANDAO**

KWA Tanzania bado hakuna aliyewahi kuelezea kinagaubaga jinsi elimu ilivyozuka na ilivyowekewa viwango, mipaka na mifumo halisi.

Tatizo la suala hilo ni kujua ni kwa kiasi gani elimu inalenga kuchangamsha akili pekee bila lengo halisi na ni wapi inajenga ufahamu halisi ambao unahitajiwa kutoka ngazi moja kwenda nyingine, kwanza kielimu halafu kimaisha.

Yako maeneo ya elimu ambayo yanawezesha kuvuka ngazi moja hadi nyingine kielimu, bila uhusiano na maisha halisi.

Suala hilo lisingeweza kujadiliwa kwa kina katika mazingira ya kusoma darasani, kupata cheti na kutafuta ajira, kwani kokote utakapokwenda hoja inakuwa ile ile, umesoma hadi ngazi gani? Hali ambayo inaamua kiasi unachoweza kuelewa majukumu ya kazi ngazi hii au ile. Mara nyingi zaidi watahiniwa hawakosei kuhusu kiwango kinachohitajika, ila kuna mazingira ya watu wengi zaidi kuwa na viwango vya elimu ambavyo havihitajiki kwa kazi wanazotafuta au wanazofanya na mara nyingine ukivitaja viwango hivyo 'unajiharibia' kupata kazi. Si inakuwa bora zaidi mtu asome aweze kufanya kazi, si zaidi?

> "Yako maeneo ya elimu ambayo yanawezesha kuvuka ngazi moja hadi nyingine kielimu, bila uhusiano na maisha halisi.

Isitoshe, licha ya kuwa mtu anakuwa na uwezo zaidi wa kufanya kazi kuliko ile anayopewa au kuhitajika kufanya, yale ambayo alisoma bila kuyahitaji kimasomo baadaye, na kutokuwapo katika dira ya kufanya au kutafuta kazi, yanapauka kichwani.

Mtu mwenye miaka 50 aliyeachia hesabu kidato cha pili lakini baadaye walilazimika kuendelea na masomo lukuki hadi kidato cha nne, akiangalia hesabu za shule za msingi anashangaa, hakumbuki lolote. Baya zaidi, hakuna mahali popote elimu hiyo inahitajiwa.

Kwa mfano ukichambua eneo ambako kuna darasa la awali, lakini walimu pia wanatoa mafunzo ya ziada, wanafanya tuisheni, ukiangalia hesabu zilizokuwa ubaoni ni sawa na zile za miongo kadhaa iliyopita.

Ndilo jambo lililoleta wasiwasi na kujiuliza mpangilio huu wa masomo ulianzia wapi na unalenga nini hasa, swali ambalo haliwezi kupatiwa majibu ya haraka. Ingebidi kuingia kwenye makumbusho ya Wizara ya Elimu kwa mfano nchini Uingereza na kuanza kufuatilia jinsi elimu ilivyokuwa, tangu enzi za umwinyi halafu kuingia karne za 'uamsho,' ubepari na leo zama za teknolojia ya kielektroniki.

Kati ya watoto waliokuwa wanafundishwa katika shule ambayo inatumia Kiingereza badala ya Kiswahili kwenye ufundishaji inawezekana wote wakaenda sekondari kwani ziko nyingi na wanapokuwa wanatumia Kiingereza tangu mwanzo kuanzia awali hadi msingi wanapata urahisi wa masomo katika ngazi hiyo ya baadaye kuliko wale wa Kiswahili.

Lakini, hata hivyo, ni wapi katika maisha ambako kijana aliyemaliza darasa la saba anahitaji kujua 'namba ndogo zaidi inayowezekana' au kupata ufafanuzi wa mlolongo na matumizi ya 'Pai 22/7' (huandikwa pi) kwanini iwepo hiyo kanuni na maana yake ni nini?

Kijana akimaliza kidato cha nne hata ingekuwa amesoma katika shule ya Kiingereza akaanza kutafuta cha kufanya, kwa mfano apendelee kujifunza ufundi wa magari, au umeme wa majumbani ndipo hoja anakuja ataitumiaje herufi 'pai'?

Hata kama angeajiriwa katika kampuni ya kuratibu matokeo ya michezo ya kubahatisha 'kubeti' na hela ambazo walioshinda hiki au kile wanaingiziwa kwenye simu, bado haielekei kuwa anahitaji kujua kuwa 'pai=3.14,' na kwanini isiwe na herufi za ziada.

Zoezi hili kuhusu pi ni kielelezo tu cha mengi yanayofunzwa katika hesabu badala ya maeneo mengine ambayo yangechangamsha akili ya mtoto na kufuatilia kujua kipi ni kipi, ila hayapo.

Hivi badala ya kufundisha jinsi ya kuhesabu pembe (angle) zote za kila aina ya mistatili uwe pembe tano, sita, saba na tisa na kuwa zote zinakuwa 'nyuzi' 360 (ni bora ingebaki degree, au digrii kwa 'tafsiri', pengine mtoto angeweza kuonyeshwa ramani ya anga za juu, zikawapo darubini, wakaangalia hata mchana?

Kuna haja gani ya kupeleka 'tablets'au kishkwambi au rula pana za kufanyia hesabu za kina au 'logarithm' wakati watoto hawajui angani kuna nini, dunia iko wapi na ndani ya bahari kukoje.

Wakati hivi kujua kiini cha mahusiano ya tarakimu, viini vya tarakimu (decimals) ni muhimu kuliko kuzielewa anga na bahari?

Ambacho si rahisi kuyakinisha ni kwanini mpangilio huu wa masomo ukaundwa na sisi tukaurithi, na tumefanya kila juhudi kuuimarisha na kuwezesha vijana wetu wafaulu, lakini kuna sintofahamu kama hiyo ni elimu au ni kuchangamsha akili?

Zaidi ya asilimia 80 ya hesabu wanazofundishwa watoto hadi sekondari hupauka wakishamaliza shule, wakati ukiangalia unakuta hesabu hizo wangeweza kuzikuta chuo kikuu mwaka wa kwanza wakazisafisha kwa haraka, halafu waendelee na hesabu za ziada.

Mtu kwa mfano aliyesoma somo la 'sets and logics' (hesabu za mafungu, mantiki) akiangalia hesabu za shule za msingi na sekondari zinafanana, wakati mwanafunzi wa chuo anahitaji kuzijua kama mtaalamu, si mtoto.

Haihitaji hadi aingie katika anga za juu, chuoni, ambako sasa ataweza kuelewa Profesa Johann Gauss mtaalamu wa hesabu na fizikia wakati akitunga nadharia hizo za hesabu ilikuwa nini.

## Mahakama Kuu inavyokuhimiza usiache kuandika wosia

**INATOKA UK.11**

Anasema, zipo hatua mbalimbali ambazo mwombaji anapitia, lakini kuna suala la pingamizi dhidi ya maombi yaliyowasilishwa na mleta maombi kuwa ama maombi yameletwa kinyume cha sheria au mleta maombi hana sifa stahiki za kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu.

"Kwa mfano, si mwaminifu, ana upendeleo, hana uwezo wa kutunza hesabu na kusimamia mali za marehemu ama ni mfujaji. Ukisoma kanuni ya 10(1) ya tangazo la serikali namba 49/1971, utagundua kuwa ndani ya miezi minne tangu kuteuliwa kwake, atapaswa kupeleka mahakamani tamko kamili na la kweli likionyesha mali na madeni yote ya marehemu kupitia fomu namba tano," anasema Kamuzora.

Anasema, kanuni ya 10(2) inatoa fursa kwa wadai, kukabidhi wosia, warithi ama wanufaika wa mirathi hiyo kupeleka ombi mahakamani kuomba kupata fursa ya kukagua au kupitia orodha na tamko hilo la mali za marehemu.

**HOFU YA WOSIA**

Kamuzora anasema, kuna dhana iliyozoeleka ndani ya jamii kwamba, kuandaa na kuacha wosia ni uchuro, hali ambayo inasababisha baadhi ya watu kutoandika wosia na wanapofariki wanaacha migogoro nyuma.

"Kila mtu ana wajibu wa kuona kuwa, kuandaa na kuacha wosia ni jambo la muhimu, ili kwamba, pale anapotwaliwa, wanaobaki wahakikishe wanasimamia wosia ama malengo ya marehemu," anasema.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# CHAWATA inavyoibua dozi kutibu matatizo ya watu wenye ulemavu

AWAMU ya tano inapoanza ni ngwe nyingine ya miaka mitano, wapo wengi wanaoitazama, miongoni mwao ni watu wenye mahitaji maalumu. Ni wale wanaoishi na ulemavu, wanawapa salamu wabunge na wawakilishi wasaidie juhudi za kuuelimisha umma utekelezaji wa sheria na mikataba ya kimataifa ya watu wenye ulemavu.

Pia, wanataka serikali kusimamia utekelezaji wa sheria na mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu, ili kuwapa haki zao za msingi kama elimu, ajira na maisha bora.

Akizungumza na Nipashe, kuhusu mambo wanayotaka serikali iwafanyie kwenye elimu na tiba, wakati huu wa awamu ya tano inapoingia kwenye kipindi cha pili, Katibu wa Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA), Mkoa wa Dar Es Salaam, Jamila Mohamed, anasema changamoto nyingi zinazowakabili watu wanaoishi na ulemavu zinasababishwa na kutokusimamiwa sheria na mikataba hiyo kufuatilia utekelezaji wake.

Anasema Sheria ya Ajira Namba 9 ya mwaka 2010 inaelekeza waajiri wote iwe sekta ya umma au binafsi kuajiri asilimia tatu ya watu wenye ulemavu kati ya watumishi 20. Ikimaanisha kuwa kila wafanyakazi 20 watatu wawe walemavu na katika wafanyakazi 100 waajiriwa wenye ulemavu wawe 15.

Jamila anasema utekelezaji wa sheria hiyo unasuasua na kuhimiza kuwe na ufuatiliaji ili kuwe na mafanikio yaliyokusudiwa.

Aidha, anaeeleza kuwa sheria za kitaifa na mikataba ya kimataifa zinasisitiza ulazima wa kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu lakini hilo halifanyiki kikamilifu.

Kwa mfano anataja ofisi nyingi za umma, shule na hospitali hazina miundombinu rafiki kwa kundi hilo jambo ambalo linawafanya Watanzania hao kuwa wanyonge linapohusu suala la kupata ajira, kusoma shuleni na vyuoni, kufikia huduma za hospitalini, hoteli na migahawa kutumia vyoo, wanawake kujifungua kwa vile kwenye wodi nyingi za uzazi mazingira si rafiki.

Jamila anaishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuboresha baadhi huduma za walemavu kama kuweka vyoo vya walemavu kwenye wodi za wazazi.

"Kwa mfano kwenye Hospitali ya Vijibweni Kigamboni ninapokaa kuna choo cha wodi ya wazazi kwa ajili ya watu wenye ulemavu hili ni jambo jema. Naishukuru serikali na kuiomba isimamie sheria na mikataba inayosisitiza kuweka mazingira rafiki." Anasema Katibu wa CHAWATA Dar.

Akizungumzia umuhimu wa kuweka miundombinu ya vyoo na sehemu za kujisitiri kwa mabinti wenye mahitaji hasa wenye ulemavu wa viungo shuleni, Jamila anataka jihudi hizo ziwafikie watoto hao ukizingatia kuwa sera ya elimu ni jumuishi.



Jamila Mohamed, Katibu Mkuu wa CHAWATA Dar es Salaam. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI**

Sera ya ujumuishi inahusisha wenye ulemavu kuchangamana na wanafunzi wengine wenye viungo vyote na kusoma pamoja bila kuwatenga wenye mahitaji maalumu, hivyo CHAWATA Dar inashauri ili sera hiyo iwe na manufaa kwa wote ni sharti miundombinu rafiki kwa walemavu iwepo kwanza.

Anakumbusha kuwa wenye ulemavu wana haki sawa na wasio na ulemavu kwenye kupata elimu hivyo serikali na wadau wazingatie hilo na kusimamia sheria na mikataba inayolinda haki na ustawi wa Watanzania hao.

Anasema changamoto kubwa ikiwamo unyanyapaa, ubaguzi na kutopata fursa za kuwawezesha kuchangia maendeleo katika jamii ni mambo ambayo hayatakiwi kupewa nafasi katika nyakati hizo za sera jumuishi na kwamba shuleni au popote kwenye ofisi za kutoa huduma wanastahili kupata na kutendewa kwa haki kama watu wengine.

### MAWASILIANO HOSPITALINI

Akizungumzia masuala ya watu wanaoishi na ulemavu katika huduma za afya, Katibu wa CHAWATA Taifa, Hamad Komboza, anasema: "Suala la mawasiliano ni muhimu kupewa kipaumbele katika kuwasiliana mathalani kuongea na wateja wenye ulemavu watoa huduma wanafahamu lugha ya alama?"

Je, matini (notes) na vipeperushi zinazotolewa mathalani hospitalini zina maandishi ya nukta nundu au breili na kwa wenye uoni hafifu maandishi yamekuzwa ili kuwasaidia wenye ulemavu.

Akijikita zaidi katika suala la lugha ya alama na ishara anashauri wahudumu wa afya kujifunza mawasiliano hayo ili kuwasaidia wasiosikia na kuzitumia ishara na alama wanapotoa huduma.

"Wakati umefika madaktari na wauguzi kujifunza lugha ya alama ili kusaidia wagonjwa wasiosikia wala kuzungumza," anasema Komboza.

Anashauri serikali kuandaa programu za kuwafundisha wahudumu hao lugha za alama na ishara ili waweze kutibu wagonjwa wenye ulemavu hasa kusikia na kuzungumza ili kuwe na usiri ambao ni msingi kwenye kutoa huduma za matibabu.

Anasema kukosekana usiri na mazingira mabovu yasiyo rafiki kunawalazimisha wagonjwa wenye ulemavu wasiende hospitalini na hivyo kukosa haki za msingi za kutunza maisha zinazopatikana kwenye matibabu.

"Mazingira yasiyo rafiki, kukosekana vyoo vya wenye ulemavu na sehemu za kunawa, wodi za uzazi zisizo rafiki, lugha mbaya za watumishi wa afya na gharama kubwa za matibabu yote haya yanawakwamisha wenye ulemavu kutumia huduma za afya," anaonya Mwenyekiti wa CHAWATA.

> Vifaa hivi ni ghali mno mfano magongo ya makwapani ni kuanzia Sh. 50,000 ambayo hutumika kwa pengine miezi sita tu, lakini yapo imara zaidi huanzia Shilingi 100,000.

### KUSAIDIWA NHIF

Komboza ananukuu Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watu (UNFPA), linalotoa takwimu za ulemavu kuwa watu wenye ulemavu ni asilimia 10 ya idadi ya watu kwenye taifa na kukisia kuwa Tanzania inaweza kuwa na wenye ulemavu takriban 6,000,000.

"Kama hivyo, ndivyo tunaomba serikali ione umuhimu wa kuwatibu wenye ulemavu kwa kuwapatia huduma za bima ya afya (NHIF) kila mmoja wetu. "Sera inasema wenye ulemavu watapata huduma za afya bure pale watakapobainika kuwa hawana uwezo. Hili sisi tunaomba libadilike. Serikali ya awamu ya tano ina uwezo imejenga reli ya mwendo kasi (SGR), miundombinu mingi ya kisasa, imeleta ndege tena si kwa mkopo tunaomba itusaidie na sisi wenye mahitaji maalumu kwa kutupa matibabu bure," anasema Komboza.

Anasema wenye ualbino wanahitaji tiba ya ngozi, mafuta maalumu ya kuwakinga na mionzi hatarishi ya jua, tiba ya macho na miwani kupitia mpango wa tiba kwa wote wenye ulemavu wataweza kupata huduma na vipimo vya magonjwa yanayowakabili kwa gharama ya serikali na wataishi kwa furaha na kuondokana na mzigo wa matibabu ambao wengi hawawezi kuubeba.

Anaamini kuwa kutokana na kutotekelezwa sheria na mikataba ya kulinda maslahi ya kundi hilo, wengi wanakuwa maskini na anaiomba serikali iwafikirie kwenye kuwapa posho (pensheni) kila mwezi mwenye ulemavu.

### KUPATA VIFAA SAIDIZI

Akizungumzia suala la kupata vifaa saidizi Komboza anasema watu wenye ulemavu wanahitaji vifaa saidizi kama magongo ya makwapani, viatu aina ya calipers, miguu bandia, viti mwendo mafuta ya wenye albino.

Mwenyekiti wa CHAWATA Taifa, anasisitiza kuwa serikali ni tajiri hivyo pamoja na kugharamia matibabu ya walemavu wote iwape bure vifaa saidizi au iweke mazingira ya kuwezesha kuvipata kwa bei ndogo na viwafikie pote mijini na vijijini.

"Vifaa hivi ni ghali mno mfano magongo ya makwapani ni kuanzia Sh. 50,000 ambayo hutumika kwa pengine miezi sita tu, lakini yapo imara zaidi huanzia Shilingi 100,000. Kuchonga miguu bandia kunaanzia Sh. 2,000,000 wakati kiti mwendo kinaanzia 500,000.

"Mafuta ya wenye ualbino ni gharama kubwa hata Sh. 100,000 kwa chupa ndogo. Viatu vya 'calipers' ambavyo mwenye ulemavu akivaa anatembea bila msaada wa magongo ni karibu Sh. 1,000,000. Tunaomba serikali itusaidie kuvipata bure au kwa gharama ndogo ambayo sote tulioko mijini na vijijini tutaimudu."

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Richter amegundua kipimo cha tetemeko kinapunguza maafa?



Uharibifu wa mali unaotokana na tetemeko la ardhi, unaweza kuwa kuangukiwa na majengo na mitambo kulipuka. Huenda kipimo cha tetemeko kikifuatwa na tahadhari kuchukuliwa mapema uharibifu unaweza kupunguzwa. **PICHA: MTANDAO**

MWANDISHI mmoja anayezungumzia kuhusu tetemeko la ardhi anasema 'tumezoea kuishi katika dunia iliyo imara hivi, kwamba dunia inapoanza kutikisika tunababaika sana.

Ni kwa sababu matetemeko ya ardhi ni mojawapo ya matukio yenye kusababisha uharibifu mkubwa zaidi duniani, ndiyo maneno hayo ni ya kweli kabisa, kwani nishati (energy) inayosababisha tetemeko kubwa la ardhi inaweza kuwa mara 10,000 zaidi ya ile ya bomu la kwanza la nyuklia.

Hata hivyo pamoja na kitisho chake, tetemeko la ardhi halikuwa na kipimo hadi mwanzoni mwa karne ya 20.

Hivyo, tetemeko la ardhi linaweza kupimwa kulingana na ukubwa au kiwango chake. Katika miaka ya 1930, mwanasayansi Charles Richter aligundua kipimo cha kuonyesha ukubwa wa matetemeko ya ardhi.

Wakati vituo vya kupima matetemeko ya ardhi vilipoongezeka, vipimo vipya vilibuniwa kwa kutumia uvumbuzi wa Richter.

Kwa mfano, kipimo cha nguvu za tetemeko la ardhi huonyesha kiasi cha nishati inayotokea kwenye chanzo cha tetemeko la ardhi.

Wakati mwingine vipimo hivyo havilingani na uharibifu uliosababishwa na tetemeko la ardhi. Kwa mfano tetemeko lililotokea kaskazini mwa Bolivia Juni 1994, lilikuwa na ukubwa wa 8.2 kwenye kipimo cha Richter na iliripotiwa kwamba watu watano walikufa. Lakini, mamia ya maelfu ya watu walikufa katika tetemeko la ardhi lililotokea mwaka wa 1976 huko Tangshan, China, ambalo lilikuwa na ukubwa wa 8.0 pekee.

> Tetemeko linaogopesha hata zaidi kwa kuwa matetemeko hayo yanaweza kutokea katika tabia yoyote ya nchi, msimu wowote na wakati wowote.

Tetemeko linaogopesha hata zaidi kwa kuwa matetemeko hayo yanaweza kutokea katika tabia yoyote ya nchi, msimu wowote na wakati wowote.

Na ijapo wanasayansi wanaweza kujua kwa kadiri fulani sehemu au mkondo ambao matetemeko yenye nguvu yanatokea au yatatokea, hawawezi kutabiri yatatokea wakati gani.Matetemeko ya ardhi hutokea kwa sababu ya kusogea kwa miamba mikubwa ambayo iko chini ya uso wa dunia.

Miamba hiyo wakati mwingine inaweza ikisababisha tetemeko la ardhi la chini ya bahari na kusababisha tsunami. Mara nyingi, mawimbi ya tetemeko la ardhi ambayo hutokea yanaweza kuwa dhaifu sana kiasi kwamba hayawezi kutambuliwa waziwazi kwenye uso wa dunia, lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ukubwa wake unaweza kutambuliwa na kurekodiwa na kipima-tetemeko maarufu kama 'Richter scale '.

Matetemeko yanasababishwa na kupasuka kwa majabali chini ya ardhi kwa hiyo mipasuko ndani ya vyanzo au sahani zinazoshikilia dunia 'tectonic plates' lakini shani hizo licha ya kusogea taratibu zinafika kipindi zinakwama kutokana na msuguano mkali hivyo, hivyo inapotokea sahani hizo zikajiondoa kwenye mkandamizo zinatikisika na kunakuwapo matetemeko makubwa duniani au baharini.

Duniani kunaelezwa kuwa kuna sahani au 'tectonic plates' saba nazo kitaalamu hufahamika kama 'African, Antarctic, Eurasian, Indo-Australian, North American, Pacific na South American.'

Ni kwa nini miamba hiyo au majabali huendelea kusongana songana? Jibu linaweza kupatikana katika dhana kuhusu sahani au mabamba yaliyo kwenye tabaka la nje la dunia 'Sasa tunajua kwamba kuna mabamba au sahani hizo saba kwenye tabaka la nje la dunia ambayo yamegawanyika katika mabamba madogo-madogo, yote hayo husongana na kwa wakati mmoja, yanaweza kusogea umbali wa milimita 10 hadi 130 kila mwaka. Matetemeko mengi ya ardhi hutokea kwenye maeneo membamba ambako mabamba au majabali hayo yametengana. Yaelekea asilimia 90 ya matetemeko makubwa ya ardhi hutokea katika maeneo hayo.

### KUJERUHI MOJA KWA MOJA

Tofauti na kipimo cha ukubwa, kiwango cha tetemeko la ardhi huonyesha jinsi linavyoathiri watu, majengo, na mazingira. Kiwango cha tetemeko la ardhi huonyesha waziwazi hasa jinsi wanadamu wanavyoathiriwa sana nalo. Matetemeko hayawajeruhi watu moja kwa moja. Badala yake, majeraha na vifo husababishwa na kuta za majengo zinazoanguka, mabomba ya gesi yanayolipuka, nyaya, vinu na mitambo ya umeme inayolipuka na vitu vinavyoporomoka ikiwamo miti inayoanguka.

Lengo moja la wataalamu wa matetemeko ni kutoa maonyo kuhusu matetemeko ya ardhi mapema. Programu ya kompyuta inayoitwa Mfumo wa Hali ya Juu wa Kuchunguza Matetemeko ya Ardhi inatayarishwa. Ripoti moja ya shirika la habari la CNN ilisema kwamba programu hiyo, pamoja na uwezo wa kupata habari haraka na pia programu nyingine tata za kompyuta, zitawasaidia wataalamu kutambua mara moja mahala ambapo mtikisiko mkubwa wa tetemeko la ardhi umetokea." Hivyo, jambo hilo litawasaidia wenye mamlaka kutuma msaada kwenye maeneo yaliyokumbwa na maafa.

Bila shaka watu wanapofahamu taarifa na kutazamia tetemeko la ardhi wanaweza kupunguza madhara, majeraha, uharibifu wa mali na zaidi ya yote kuokoa maisha. Hata hivyo, matetemeko ya ardhi yanaendelea kutokea. Hivyo, swali linalozuka ni hili watu wamesaidiwaje kukabiliana na hasara?

Kipima tetemeko ni chombo kinachotumiwa kupima na kurekodi mtikisiko wa ardhi wakati tetemeko la ardhi linapotokea. Kipimatetemeko cha kwanza kilibuniwa mwaka wa 1890, duniani leo kuna vituo zaidi ya 4,000 vinavyopima matetemeko ya ardhi.

**MITANDAO**

## Machinga wafunguka taarifa za uzushi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MACHINGA wilayani Dodoma wamelaani taarifa za upotoshaji zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuwa watabomolewa vibanda vyao na Halmashauri ya Jiji la Dodoma baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu 2020.

Tamko hilo lilitolewa na viongozi hao wakati wakizungumza na waandishi wa habari, kuhusu uvumi unaosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imepanga kubomoa vibanda vyao.

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Machinga, Wilaya ya Dodoma, Bruno Mponzi, alisema taarifa hizo zinatakiwa kupuuzwa kwa kuwa ni za upotoshwaji ambazo zinalenga kuwagombanisha na serikali kupitia halmashauri ya jiji.

"Sisi machinga wa Jiji la Dodoma, tunaipongeza serikali yetu kwa ushirikiano mkubwa tunaofanyiwa ikiwa ni pamoja na kututhamini kutupatia elimu ambayo imetuwezesha kufanya kazi zetu kwa mujibu wa sheria na kufanya shughuli zetu kwa uhuru muda wote," alisema.

Katibu wa umoja huo wa machinga, Anna Ndaga, aliwataka wafanyabiashara ndogo kupuuza taarifa hizo kwa kuwa ni uzushi.

"Baada ya watu kusikia kuwa rais wetu ana malengo makubwa ya kuboresha na kutusaidia kupata mikopo kupitia vitambulisho hivyo, wanaanza kuzusha mambo ambayo wanataka kutugombanisha na serikali yetu," alisema.

Alisema kuwa watu hao wanatakiwa kupuuzwa kwa kuwa hawawatakii mema machinga kwa kutoa taarifa za zisizo za kweli.

Christian Msumari, alisema kuwa kwa elimu kubwa waliyoipata kutoka halmashauri ya jiji, hawafikirii kuona machinga wakibomolewa vibanda vyao kwa kuwa wanaheshimu maelekezo yanayotolewa.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema kuwa halmashauri ya jiji hilo, kazi yake sio uvunjaji wa vibanda bali inafanya utoaji wa elimu ya kuwasaidia kujiepusha kufanyabiashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Alisema halmashauri hiyo haina mpango wa kuwabomolea kama taarifa zilivyoenea kwenye mitandao ya kijamii.

# TAKUKURU yaasa wanafunzi kukimbilia mafanikio

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imewaasa wanafunzi wanaotaka mafanikio ya haraka kuacha na badala yake wafanye kazi kwa bidii, ili kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, aliyasema hayo juzi wakati wa mahafali ya wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari ambao ni wanachama wa klabu za kupinga rushwa.

Kibwengo, alisema uvivu wa kufanya kazi au kusoma kwa bidii ni moja ya chanzo cha kusababisha kujiingiza katika vitendo vya rushwa suala ambalo halikubaliki kisheria.

Alisema, kinachotakiwa hivi sasa ni kila mmoja kuhakikisha anaendelea kujisomea na kufanya kazi ikiwamo kutoa elimu kwa vijana wenzao ambao hawana uelewa kuhusu rushwa ili kuitokomeza.

"Tunaomba mkawe mabalozi wazuri katika utoaji elimu ya kujikinga na rushwa, tunahitaji kuona vijana wanatambua nini maana ya rushwa na namna ya kujikinga," alisema Kibwengo.

Alisema wakianza kupambana na rushwa tangu wakiwa wadogo, itawarahisishia watakapokuwa ofisini hawataiendekeza.

Pia, alisema wanafunzi hao ambao ni wanachama wa klabu hizo, wamekidhi vigezo vya kuitwa wanachama na nafasi hiyo wakaitumie vizuri kuhakikisha wanafanikisha kufikisha ujumbe wa kujikinga na vitendo hivyo.

Akizungumzia maofisa wa TAKUKURU kupita katika shule mbalimbali kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa walimu walezi, alisema suala hilo watalifanyia kazi ili kuziboresha klabu hizo.

Vile vile, alisema mafunzo kwa walimu na walezi wa klabu katika shule wanazosoma ni muhimu kupewa kwa sababu wao ndio wanaokaa nao muda mwingi na wanafunzi.

Aliwataka wahitimu hao wanapokuwa uraiani kusaidia kutoa taarifa wanapoona kuna vitendo vya rushwa ya ngono ili taasisi hiyo izifanyie kazi taarifa.

Alisema, uwezo wa kupambana na rushwa waliouonyesha wakati wakiwa shuleni wakauonyeshe pia uraiani, kwa sababu baadhi ya jamii wanaficha taarifa za rushwa ya ngono na nyingine na kusababisha ugumu wa taasisi hiyo kumkamata muhusika wa kitendo hiko.

Alisema wanafunzi hao kama mabalozi wanapaswa kuongea, kukemea, kuelimisha na kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa.

Hata hivyo, alisema kuwa mitaani ndio kuna vitendo vya rushwa ya ngono na nyingine na kwamba wakitumia vizuri uanachama wao wa klabu za kupinga vitendo hivyo, watasaidia kuitokomeza.



Mratibu wa Elimu Jumuishi Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma kutoka kanisa la Free Pentecost, Jane Mgidange, akizungumza na baraza la watoto wenye ulemavu, kamati ya malezi na kikundi cha wazazi kwenye mafunzo ya ushawishi na utetezi, yaliyofanyika wilayani humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanawake wahamasishwa kuchangamkia fursa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya wanawake kutoka vyama vya siasa nchini (T-WCP-Ulingo), imewataka wanawake nchini kuchangamkia fursa mbalimbali ambazo zinatolewa na serikali ya awamu ya tano.

Mjumbe wa sekretarieti ya Ulingo, Saum Rashidi, alitoa rai hiyo jana jijini hapa wakati alipokua akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hotuba iliyotolewa na Rais John Magufuli, wakati wa kuzindua Bunge la 12.

Alisema, wanawake wanaipongeza serikali kwa kuwapa nafasi kubwa za maamuzi.

"Tunaipongeza serikali yetu ya awamu ya tano kwa kuthamini mchango wa wanawake katika jitihada mbalimbali za kuleta maendeleo," alisema.

Alisema katika uongozi wa awamu ya tano imefanya mambo mengi ambayo yamewainua wanawake katika kushiriki kuleta maendeleo ya taifa.

"Serikali hii tunaipongeza sana kwa kutambua umuhimu wa wanawake na kuwapatia nafasi kubwa za maamuzi, lakini pia zipo fursa mbalimbali zilizotengezwa ambazo wanawake wanatakiwa kuzitumia ili kujikwamua kutoka hapa walipo sasa," alisema Rashidi.

Akizungumzia hotuba ya kulizindua Bunge la 12, alisema kuwa wanampongeza Rais Magufuli, kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni mambo muhimu ambayo ni dira ya taifa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema, kitendo cha Rais Magufuli, kuamua kujenga shule moja ya masomo ya sayansi ya wasichana kila mkoa, imeonyesha ni jinsi gani ambavyo amedhamiria kuwainua wanawake.

"Hii itasaidia pia kuongeza idadi ya wanawake ambao ni wataalamu wa mambo ya sayansi nchini jambo ambalo linatupa faraja sisi wanawake wa kitanzania pia shule hizi zitasaidia kupunguza tatizo la mimba kwa wanafunzi wa kike," alisema.

Vile vile, alisema kuwa serikali kuendelea kugharamia elimu ya msingi hadi kidato cha nne itasaidia kuwaondolewa adha wazazi ambayo wangepata katika kulipia elimu.

Pia, alisema kuwa wanaipongea Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa kusimamia uchaguzi mkuu na kutumia kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ufanisi.

"Katika uchagauzi mkuu 2020, kiasi cha fedha kulichotengwa ni Sh. bilioni 361, lakini Tume wametumia Sh. bilioni 262 kiasi kilichobaki kinaweza kwenda kushughulikia mambo mengine," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Taifa wa Chama cha ADA -TADEA, Ziada Athumani, aliwata wanawake kuchangamkia fursa ikiwamo mikopo isiyokuwa na riba ili kuanzisha miradi mbalimbali itakayowakwamua kiuchumi.

Aliwataka Watanzania kuilinda amani kwa kuwa kama ikitoweka watu watakaoathirika zaidi ni kinamama na watoto.





# Mbeya yatenga bil. 1/- mikopo vikundi wanawake na vijana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetenga shilingi bilioni moja katika mwaka wa fedha 2020/2021, zitokanazo na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuendeleza shughuli za uzalishaji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa jiji hilo, Beatha Mtani, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa robo ya kwanza ya Mradi wa Kuongeza Shughuli za Uzalishaji na fursa za ajira kwa vijana unaotekelezwa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la SHOP, chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la The Foundation for Civil Society.

Alisema fedha zilizotengwa ni ongezeko la zaidi ya Sh. milioni 300 ya zile zilizokuwa zimetolewa katika mwaka wa fedha 2019/2020, zaidi ya Sh. milioni 600 ambazo zilitolewa kwa vikundi 85.

Aliwataka vijana wanaowezeshwa na Shirika la SHOP kuchangamkia mikopo hiyo ambayo haina riba ili wakuze shughuli zao na kupunguza tatizo la ajira pamoja na umaskini kama ilivyo lengo la shirika hilo na serikali kwa ujumla.

Alisema pia kuna mashirika mengine likiwamo la kuhudumia viwanda vidogo nchini (SIDO) ambayo yanatoa mafunzo na kuendeleza ubunifu.

"Sharti kubwa la vijana kupata mikopo hii ya halmashauri ni kuunda vikundi vya watu wasiozidi umri wa miaka 35 na kikundi hicho lazima kiwe na miradi ambayo ni endelevu, lakini kabla hatujatoa mkopo huo ni lazima tukitembelee kikundi husika," alisema.

Alilipongeza shirika hilo kwa kujitolea kutoa elimu kwa vijana hao na kwamba elimu hiyo imeongeza mwamko wa vijana kujitokeza kuomba mikopo na katika mwaka wa fedha uliopita vikundi 30 vya vijana vilijitokeza kuomba mikopo hiyo na vikapata.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la SHOP, Maria Dominick, alisema mradi huo ni wa miezi sita na unatekelezwa katika kata 15 kati ya 36 za Jiji la Mbeya.

Alisema katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo, vikundi vya vijana vimepata mafanikio makubwa ikiwamo kupata maeneo ya kufanyia shughuli zao za usindikaji na uuzaji wa bidhaa mbalimbali.

Alisema baadhi ya vijana wamepatiwa chumba cha kusindikia bidhaa kwenye majengo ya SIDO na kwenye Soko la Kimataifa la Mwanjelwa wamepata chumba cha kuuzia bidhaa wanazozalisha.

"Pia vijana hawa walishiriki kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane) mwaka huu na walionyesha bidhaa mbalimbali ambazo wanazalisha, pia kuna kikundi cha vijana wa maparachichi cha Iziwa walifanya kazi kubwa sana," alisema Maria.

Ofisa ufuatiliaji wa miradi wa shirika hilo, Amina Mwakalobo, alisema awali vijana hao walikuwa wanazalisha bidhaa zao kwa wingi, lakini wakawa wanakosa maeneo ya kuuzia.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la SHOP, Maria Dominick (kushoto), akitoa tathmini ya utekelezaji wa mradi wa kuongeza shughuli za uzalishaji na fursa za ajira kwa vijana jijini Mbeya, wakati wa mkutano wa tathmini ya robo ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wananchi walalamika mafuriko kuwaathiri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuboresha mitaro ya maji ili kupunguza mafuriko yanayowaathiri mara kwa mara.

Waliyasema hayo jana walipokuwa wanaongea na Nipashe baada ya mvua kuanza ambapo walisema baadhi ya mitaro ilifukiwa wakati wa upanuzi wa barabara na kusababisha maji kusambaa kwenye makazi ya watu.

Mmoja wa wananchi hao, Tilson Kamwela, alisema mvua imenyesha siku moja na madhara ya mafuriko yameanza kuonekana kutokana na maji kuingia kwenye nyumba za watu na kuhatarisha maisha yao.

Alisema mitaro isipoboreshwa mapema kuna hatari ya baadhi ya wananchi kukimbia makazi yao na baadhi ya nyumba kubomoka.

"Kuna baadhi ya maeneo hapa maji yamekosa mwelekeo kutokana na mitaro kufukiwa na mkandarasi aliyekuwa anapanua barabara hapa, sasa mvua hii imenyesha siku moja, lakini maji yameingia na maeneo ambayo hayajawahi kuingia," alisema Kamwela.

Naye Neema Mwanja ambaye ni mmiliki wa mgahawa katika eneo la Tarafani, alisema maji yanaingia mpaka kwenye vyumba vyao na hivyo kusababisha biashara kukwama kutokana na wateja kukimbia.

Alisema hata mitaro iliyopo mingi ni ya zamani na haina uwezo wa kuhimili wingi wa maji yanayojaa wakati wa mvua na kuomba ipanuliwe na iliyofukiwa ifukuliwe na kunyooshwa.

Aliiomba serikali pia kuwadhibiti baadhi ya wafanyabiashara wanaotupa taka kwenye mitaro iliyo jirani na maeneo yao ya biashara na kusababisha kuziba.

# Waliohitimu mgambo waonywa kutumia ubabe

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, imewataka vijana waliohitimu mafunzo ya mgambo kuepuka kuzitumia mbinu za kijeshi walizofundishwa ikiwamo kuwaonea wananchi na badala yake wazitumie mbinu hizo kwa manufaa ya umma.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafunga mafunzo ya mgambo ambayo kwa wilaya hiyo yalifanyika katika Kata ya Mbugani na kushirikisha zaidi ya vijana 200.

Aliwataka vijana hao kuwaongoza wananchi wa maeneo wanayoishi kuhakikisha wanaishi kwa kufuata taratibu za nchi na kushirikiana na vyombo mbalimbali vya dola kulinda amani kwenye maeneo yao kwa kuwadhibiti wahalifu.

Mayeka alisema vijana hao hawatakiwi kuonyesha ubabe kwa wananchi kwa kutumia mafunzo waliyoyapata kwa kuwa kufanya hivyo ni kulichafua jeshi.

"Mmepata mafunzo ya ukakamavu, sasa usije ukafika mtaani ukataka watu wakujue kwamba wewe umepata mafunzo unajua kupiga kareti, unajua kupiga mitama na wewe ndiyo wewe, hatutarajii kabisa kusikia hayo," alisema Mayeka.

Aliwasisitiza vijana hao kufanya kazi kwa weledi, ili kuisaidia serikali na kuonyesha umuhimu wa mafunzo hayo ili yasigeuke kuwa kero kwa wananchi.

Awali, vijana hao waliiomba serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya mafunzo hayo ili yawafikie wengi zaidi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini kwa kuwa yanawasaidia kupata ajira.

Vilevile, walisema mafunzo hayo yanawasaidia vijana kupata ajira na kuwa na shughuli ambazo zinasaidia kupunguza matukio ya uhalifu mitaani.

Mmoja wa vijana hao, Rabana Ndumbaro, mkazi wa Kijiji cha Mbugani, alisema mafunzo hayo yanawasaidia kuongeza ulinzi kwenye vijiji vyao hasa kukabiliana na matukio ya uhalifu.

Pia, alisema yanawasaidia kukabiliana na tatizo la ajira kwa kuajiriwa kwenye kampuni za ulinzi ambazo kwa sasa ili kijana aajiriwe ni lazima awe amepitia mafunzo ya mgambo ama mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

"Sasa hivi tuna ujuzi ambao utatusaidia kupata ajira na kupunguza ukali wa maisha, tunategemea kuyatumia mafunzo haya kuongeza ulinzi hata kwenye maeneo yetu kwa kukabiliana vilivyo na wahalifu," alisema Ndumbaro.

Mshauri wa Jeshi la Akiba wa Wilaya ya Chunya, Magandeka Mwakimila, alisema awali wakati mafunzo hayo yanaanza vijana walikuwa 207, lakini waliofanikiwa kufika mwisho ni 139 baada ya wengine kuishia njiani.

Alisema baadhi ya vijana hao walishindwa kuhitimu mafunzo hayo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utovu wa nidhamu pamoja na maradhi na kati ya waliohitimu wanawake ni 40.

Vijana hao walifundishwa mambo mbalimbali ikiwamo kukabiliana na rushwa, mafunzo ya polisi, usalama barabarani, somo la Uhamiaji, mafunzo ya zimamoto na huduma ya kwanza.



Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, akiwasilisha mada inayohusu uhusiano wa Baraza la Wawakilishi na mihimili mingine katika mafunzo elekezi kwa wajumbe wa baraza hilo, yaliyofanyika Chukwani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

# 16 wafariki dunia ajali za barabarani mwezi mmoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU 16 wamefariki dunia kati ya 23 waliopata ajali za barabarani kwa mwezi Oktoba mwaka huu, Zanzibar.

Hayo yalielezwa wakati wa uwasilishaji wa ripoti ya takwimu za ajali na makosa ya barabarani kwa mwezi huo, uliofanyika Ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mjini Unguja.

Akiwasilisha ripoti hiyo, juzi mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Asha Mussa Mahfoudh, alisema miongoni mwa waliofariki wanaume ni 14 na wanawake wawili huku Wilaya ya Magharibi 'A' ikiongoza ikiwa na ajali tano.

Alisema, idadi ya ajali kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 109.1 kutoka ajali 11 mwezi Septemba 2020 hadi 23 kwa mwezi Oktoba 2020.

Aidha, alisema jumla ya makosa ya barabarani 1,118 yameripotiwa mwezi Oktoba ambayo yote yalifanywa na wanaume kutokana na kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani likiwa kosa kuu, makosa 279.

Alisema, Wilaya ya Magharibi 'B' ilikuwa na idadi kubwa ya makosa 296 sawa na asilimia 26.5 kati ya makosa yote.

"Lakini Wilaya ya Micheweni ilikuwa na idadi ndogo ya makosa mawili pekee," alisema. Naye Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Makosa ya Uhalifu Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Khamis Mwinyi Bakari, alisema, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mamlaka zingine zinaendelea kutoa elimu kwa madereva na waendesha pikipiki ambao ndiyo wanaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha ajali nyingi za barabarani.

Ofisa Leseni Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Nassor Mwinyi Mzale, aliwataka wamiliki na waendesha pikipiki kufuata utaratibu unaowataka kuwa na leseni za udereva pamoja na kuzingatia matumizi sahihi ya alama za barabarani.

Kwa upande wake Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Magharibi 'B', Jabiri Hassan, alisema, pamoja na jitihada zinazofanywa na Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani, waendesha bodabado wanachangia ajali nyingi za barabarani kwa kutofuata miongozo ya uendeshaji salama.

# Jaji Mkuu aeleza umuhimu mihimili ya dola kushirikiana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, amesema kuna umuhimu mkubwa wa mihimili mitatu ya dola kushirikiana katika utendaji wa kazi zao, ili kuwahudumia vizuri wananchi katika kuwaletea maendeleo.

Jaji Makungu aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha mada ya "uhusiano wa Baraza la Wawakilishi na mihimili mingine katika mafunzo elekezi kwa wajumbe hao yanayoendelea katika ukumbi wa baraza hilo Chukwani.

Alisema lengo kubwa la vyombo hivyo ni kugawana madaraka katika kutoa huduma bora kwa wananchi katika misingi ya demokrasia, na kwamba malengo hayo hayatofikiwa ikiwa vyombo hivyo vitakuwa na migogoro.

Alieleza kuwa kwa upande wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, vyombo hivyo vitatu (Mahakama, Bunge/ Baraza la Wawakilishi na Serikali) vinafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa ambao yameipelekea serikali kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wake.

Wakati huo huo, Balozi mstaafu, Dk. Mahadhi Juma Maalim, akiwasilisha mada mgawanyo wa madaraka na kazi za Baraza la Wawakilishi, aliwasisitiza wajumbe wa baraza hilo kujifunza kwa umakini sheria na kanuni zinazoongoza utendaji wa kazi wa baraza.

"Pia muwatumie wataalamu wa baraza hilo kutekeleza majukumu yao kwa uweledi mkubwa.

# 23,600 kufanya mtihani kidato cha 4

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI 23,621 wanatarajiwa kufanya mtihani wa kidato cha nne Zanzibar kwa mwaka huu, unaotarajiwa kuanza Novemba 23.

Akitoa taarifa jana kuhusu mitihani hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Sekondari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi Issa, alisema kati ya watahiniwa hao wanawake ni 14,016 sawa na asilimia 59.3 na wanaume ni 9,605 sawa na asilimia 40.7.

Asya alisema Zanzibar itakuwa na jumla ya vituo 232, ambapo kati ya hivyo vituo 172 sawa na asilimia 74.1 ni vya serikali na vituo 60 sawa na asilimia 25.9 ni vya binafsi.

Aidha, aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao na kuwapa nasaha nzuri kuhusu kufanya vizuri katika masomo na kuwasisitiza wanafunzi kufika shule kwa wakati na kujiepusha na vitendo vya udanganyifu wakati wa mitihani yao.

Pia aliwaomba walimu kutowawekea kinyongo wanafunzi kwa njia yoyote na badala yake kuwasamehe pale walipowakosea pamoja na kuwapa baraka zao, ili kufaulu vizuri mitihani yao na kujiendeleza zaidi kimasomo hapo baadaye.

Mkurugenzi huyo aliwaomba madereva na makondakta wa daladala kuwapa msaada zaidi wanafunzi hasa katika kipindi hiki wanachofanya mitihani kutokana na mvua kunyesha ili kuwahi na kufanya mitihani yao kwa wakati.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, aliwataka wanafunzi wa Shule ya Umoja Uzini kujiandalia mazingira yao ya baadaye kwa kusoma kwa bidii ili kufaulu mitihani yao ya kidato cha nne inayotarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu.

Akizungumza na wanafunzi hao wanaojiandaa kufanya mitihani yao ya taifa, alisema kuwa elimu ndio dira ya maisha ya kila mwanafunzi hivyo ni vyema wakujitahidi kwa bidii ili kufikia malengo yao waliojiwekea ya kielimu.

Ayoub aliwapongeza wanafunzi hao kwa kuonyesha ari na bidii kwa kutumia muda wao katika kujisomea masomo ya ziada, hali ambayo inakwenda sambamba na azma ya serikali ya mkoa huo ya kuongeza idadi ya ufaulu wa daraja la kwanza na kutokomeza wimbi la wanafunzi wanaopata sifuri.

Aidha, alisema serekali itaendelea na jitihada zake za kuandaa mazingira bora ya elimu ikiwamo kujenga shule za kisasa pamoja na vifaa vya masomo ya sayansi, ili kutoa wataalamu watakaoweza kulisaidia taifa katika nyanja mbalimbali katika jamii.

Katika hatua hiyo, aliwaagiza watendaji wa Wilaya ya Kati kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi hao kwa haraka kwa lengo la kuwafanya waweze kusoma katika mazingira bora, ili kutimiza ndoto zao za kielimu.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Umoja Uzini, alisema lengo la kuanzisha kambi kwa watahiniwa hao ni kuwapatia muda wa kutosha kupitia masomo yao.

Kwa upande wao wanafunzi walimwahidi Mkuu wa Mkoa huyo, kwamba watahakikisha wanasoma kwa bidii ili kufanya vyema katika mitihani, huku wakieleza kuwa watafanya mitihani hiyo bila ya kufanya udanganyifu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

*NIPASHE NI JIBU LAKO*
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI

**ANDREA JOHN FIDELI** amepotelewa na kadi zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Kadi ya Pikipiki **Namba 115922470,** Kadi ya **Tin No. 125-039-162** na Kadi ya Sumatra, tayari taarifa ya upotevu huo umesharipotiwa Kituo cha Polisi Lindi mjini. Naomba yeyote atakayeiona na kuviokota avipeleke Kituo chochote cha Polisi au awasiliane kwa Namba ya **Simu 0712 822 949.**

**IJAMU COMPANY LIMITED**
**NAMBA YA KAMPUNI : 5982**
**YAH: TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI**

Kufuatia maamuzi ya Bodi ya wakurugenzi na wanahisa wa IJAMU CO.LTD imeamuru kufunga shughuli zake za biashara kuanzia tarehe 30/10/2020.

Kwa tangazo hili watu wote ambao wanaidai IJAMU CO.LTD wapeleke madai yao ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili katika ofisi za **IJAMU CO.LTD**

**Kwa mawasiliano wamuone:**
**Mkurugenzi: IDDI JACKSON MULENGA (0754-595808)**
**: SAIDI IDDI MULENGA (0768-078570)**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**DAUDI SAMWELI NYAGAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA COASTER** yenye namba za usajili T.247 BKK.Chassis namba JT74BB4207000995.Engine namba 14B15033655.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi:**
**MBE/MBA/RB/683904/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KAM CONSTRUCTION CO. LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 976 AXJ. AINA YA PIKIPIKI: GSM. RANGI YA PIKIPIKI: NYEKUNDU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi:

**Taarifa ya polisi:**
**DSM/PHQ/RB/737607/2020.**
**Au apige simu namba 0767585508.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**
**MADAI NAMBARI 125 ya 2020**
**Mdai LUCY GODBLESS SHOO**
**amdai**
**Mdaiwa HILARY JOSEPH**
**HILARY JOSEPH**
**ARUSHA**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai).
UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI KUJIBU LALAMIKO LA MADAI YA TALAKA.
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi kufika mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 23/11/2020 saa 08:30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Endapo hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16/11/2020.

**Hakimu wa Mahakama**

## KUPOTEA KWA VYETI



Mwenye picha hapo juu


**MBUKE MARCO NZELLA**

Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha nne chenye **namba S.0235-0101** kilichotolewa na baraza la mitihani mwaka **2012 BUKUMBI SEKONDARI.**

Cheti cha Ualimu kilichotolewa **NG'WANZA TEACHERS COLLAGE mwaka 2015.**

Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **ARU/ARU/RB/793644/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



Mwenye picha hapo juu

**MBUKE MARCO NZELLA**

Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha nne chenye **namba S.0235-0101** kilichotolewa na baraza la mitihani mwaka **2012 BUKUMBI SEKONDARI.**

Cheti cha Ualimu kilichotolewa **NG'WANZA TEACHERS COLLAGE mwaka 2015.**

Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **ARU/ARU/RB/793644/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Mussa Ramadhani Mussa Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya Nissan Caravan yenye namba za usajili T976 DUR Chassis No: CWGE24406703 ,Engine No: 0032039574 yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **RB No. TAN/RB/789374/2020**

**KATIKAN MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na…..81 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**INOCENT FRANK MREMI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**NEEMA RICHARD LYIMO**

**TARIFA YA KAWAIDA**

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji/waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 3 mwezi wa December mwaka 2020.

## KUPOTEA KWA CHETI



**RABIA A. MDOE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2421-0028** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **STAR HIGH SCHOOL mwaka 2017**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: ARU/ARU/RB/787287/2020.**

## KUPOTELEWA KWA KADI ZA GARI

**RAGNAR HEDTJARN** anatangaza kupotelewa na kadi tatu za gari **VOLKSWAGEN** yenye namba za usajili T 593 **AUU,TOYOTA HILUX T 846 ACR , FORD T 229 ASE.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/793095/2020.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wanajeshi Ethiopia waukomboa mji mwingine

**ADDISABABA,** Ethiopia

IMEELEZWA kuwa wanajeshi wa Ethiopia wamefanikiwa kuukomboa mji wa Alamata ulipo katika mkoa wa Tigray.

Serikali ya Ethiopia imeeleza hayo huku ikiwashutumu viongozi wa jimbo hilo kwa kuwafungulia wafungwa 10,000 katika mji huo walipokuwa wakikimbia.

Limeeleza kuwa, wakati wapiganaji wa chama kinachotawala katika Jimbo la Tigray- TPLF, waliposhindwa katika mji wa Alamata, walitoroka wakiwa pamoja na wafungwa 10,000.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinaeleza kuwa hapakuwa na kauli ya moja kwa moja kutoka kwa viongozi wa Tigray, kuhusiana na matukio katika mji wa Alamata.

Alamata ni mji ulio takriban kilomita 120 mbali na mji mkuu wa Tigray Mekelle, lakini ulio karibu na mpaka wa Jimbo la Amhara.

Wakati hayo yakijiri, kiongozi wa jimbo hilo linaloasi la Tigray, Debretsion Gebremichael, ameuhimiza Umoja wa Mataifa (UN), pamoja na Umoja wa Afrika (AU), kuishutumu serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed, kwa kutumia silaha nzito zikiwamo ndege zisizokuwa na rubani, wakati wa operesheni yake ya kijeshi ambayo imedumu kwa wiki mbili sasa.

Gebremichael alisema Abiy anaendeleza vita dhidi ya watu wa Tigray na ndiye wa kuwajibika kufuatia dhiki ya makusudi dhidi ya raia pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu kama bwawa la Tekete na kiwanda cha sukari cha Wolkait.

Kumekuwa na maandamano pia ya kulaani machafuko yanayoendelea huku wakitoa miito ya usitishaji vita.

Siku ya Jumamosi, vikosi vya Tigray vilifyatua roketi kuelekea nchi jirani ya Eritrea, hivyo kuzidisha machafuko ambayo yamedumu kwa zaidi ya siku 13 sasa.

Mgogoro huo tayari umesababisha vifo vya mamia ya watu katika pande zote mbili zinazozozana, hali inayotishia utulivu wa maeneo mengine ya Ethiopia. **DW**

# Rais Museveni ateuliwa mpatanishi amani Ethiopia

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, atasimamia mazungumzo ya kuleta amani nchini Ethiopia, kati ya serikali na maofisa wa eneo la Tigray.

Taarifa iliyotolewa na maofisa wa serikali ya Ethiopia walisema kwamba mazungumzo hayo yamepangwa kuanza muda wowote kuanzia sasa, kaskazini mwa Uganda.

Naibu Waziri Mkuu wa Ethiopia, Demeke Mekonnen Hassen, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje, pamoja na wawakilishi wa Tigray, alisema maofisa hao wanatarajiwa kufika nchini Uganda kwa mazungumzo hayo.

Hayo yanajiri wakati kiongozi wa eneo lililojitenga nchini Ethiopia, Tigray, amethibitisha kwamba wapiganaji wake walifanya mashambulizi ya roketi kwenye Uwanja wa Ndege katika mji mkuu wa Eritrea.

**Shambulizi hilo linaongeza wasiwasi wa kusambaa kwa vita katika eneo hilo la pembe ya Afrika.**

Shambulizi hilo linaongeza wasiwasi wa kusambaa kwa vita katika eneo hilo la pembe ya Afrika.

Debretsion Gebremichael, alisema kwamba wapiganaji wake walishambuliwa kila upande na maelfu ya wanajeshi wa Eritrea na vifaru anavyodai waliingia Tigray kuwasaidia wanajeshi wa Ethiopia.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy, aliandika ujumbe wa Twitter kwamba Ethiopia ina uwezo wa kutosha kufanikisha malengo yake katika eneo la Tigray bila msaada wowote, lakini hakujibu moja kwa moja madai ya Debretsion.

Mwanadiplomasia mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani kwa Afrika, Tibor Nagy, alishutumu mashambulizi ya vikosi vya Tigray dhidi ya Eritrea na kulaani kile alichokiita juhudi zao za kuufanya mzozo huo kuwa wa kimataifa.

Abiy alizindua kampeni hiyo Tigray Novemba 4, mwaka huu baada ya kushutumu vikosi vya eneo hilo kwa kushambulia wanajeshi wa serikali kuu, walio katika Jimbo la Kaskazini, ambalo linapakana na Eritrea na Sudan.

Idadi ya watu ambao wamekimbilia Sudan kutokana na mzozo huo kaskazini mwa Ethiopia imeongezeka hadi 20,000, shirika la wakimbizi la Umoja wa Mataifa na maofisa wa eneo hilo walisema Jumapili. **VOA**




Waandamanaji nchini Peru, wengi wao wakiwa vijana wameingia mitaani kuipinga serikali ya mpito ya Manuel Merino. **PICHA: BBC**

# Waziri Merino ajiuzulu baada ya maandamano

**LIMA,** Peru

WAZIRI wa mpito wa Peru, Manuel Merino, amejiuzulu baada ya watu wawili kufariki dunia wakati wa maandamano dhidi ya serikali.

Merino, ambaye ni spika wa zamani wa Baraza la Congress, alikuwa madarakani katika kipindi cha wiki moja.

Alichukua nafasi ya Rais Martín Vizcarra baada ya kuondolewa madarakani na bunge Jumatatu kwa madai ya hongo, ambayo aliyakanusha.

Wanasiasa wa ngazi ya juu walikuwa wametoa wito wa kujiuzulu kwa Merino, kufuatia mashambulio dhidi ya waandamanaji dhidi yake.

Mawaziri 12 kutoka katika baraza lake alilokuwa amelichagua hivi karibuni alijiuzulu mapema siku ya Jumapili kupinga ukatili unaofanywa na polisi na namna rais anavyoshughulikia mzozo.

Maelfu ya waandamanaji wengi wao wakiwa vijana walishiriki katika maandamano ya kumpinga Vizcarra. Walilishitumu Bunge la Congress nchini humo kwa kupanga mapinduzi ya bunge.

Vizcarra (57) alikuwa akipata uungwaji mkono miongoni mwa wapigakura walio wengi, kwa majaribio yake ya kuleta mageuzi.

Maandamano yaliyotokea mwishoni mwa wiki mjini Lima yalikuwa ya amani, lakini makabiliano yakaibuka majira ya jioni baina ya polisi na waandamanaji.

Polisi wanaripotiwa kufyatua mabomu ya machozi na risasi dhidi ya waandamanaji ambao baadhi yao walikuwa wkiwarushia mawe na vijinga vya moto.

Kwenye makabiliano hayo, watu wawili mmoja mwenye umri wa miaka 24 na mwingine miaka 25, waliuawa. Maofisa wa afya wanasema kuwa walikufa kutokana na risasi.

Katika hotuba yake, Merino alisema: "Ninataka nchi nzima itambue ninajiuzulu."

Hofu ya kisiasa inaendelea kutanda huku Peru ikikabiliwa na mdororo wa uchumi uliosababishwa na janga la ugonjwa wa virusi vya corona.

Peru ilitangaza amri ya kukaa nyumbani katika eneo la Amerika Kusini, ili kuzuwia kusambaa kwa virusi vya corona, lakini bado imekuwa ikishuhudia ongezeko la juu la idadi ya watu wanaoambukizwa ugonjwa huo.

Hadi sasa imeripoti kuwa watu 935,000 wameambukizwa maradhi hayo na wengine 35,000 wamekufa, kwa mujibu wa takwimu za Chuo Kikuu cha Johns Hopkins University, kulifanya taifa hilo kuwa na theluthi moja ya kiwango cha vifo kwa watu 100,000 duniani.

Merino amekuwa akitarajia kubaki mamlakani hadi Julai 2021 wakati muhula wa Vizcarra ungemalizika.

Vizcarra alikuwa katika malumbano makali na Congress, ambalo lina wabunge wengi kutoka vyama hasimu, tangu alipoingia madarakani Machi, 2018. **BBC**

# LA LIGA KUBWA KULIKO MESSI – FORLAN




**MADRID,** Hispania

DIEGO Forlan ametupilia mbali umuhimu wa nyota wa Barcelona, Lionel Messi kubaki kwenye LaLiga, akisisitiza ligi hiyo itaendelea kutamba bila ya uwapo wa mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

Majaliwa ya Messi yamebaki kuwa mjadala muhimu pale Barca baada ya kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka mwishoni mwa msimu wa 2019-20.

Nahodha huyo wa Barca alikuwa akitajwa kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu ya Manchester City kabla ya kuamua kubaki kule Hispania, ingawa pia amekuwa akihusishwa na mabingwa wa Ligue 1, Paris Saint-Germain na Inter Milan.

"Siwezi kusema kwamba yeye ni zawadi (Messi amebaki)," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Atletico Madrid, Forlan, ambaye alishinda taji la Europa na UEFA Super Cup wakati wa kipindi chake akicheza pale Madrid kati ya mwaka 2007 na 2011, akiiambia Marca Sport.

"Kwa kawaida LaLiga imekuwa shukrani kwa wachezaji wakubwa ambao wamecheza katika klabu tofauti. Lakini LaLiga ni LaLiga, na klabu ni muhimu sana, na wapo kwenye historia.

"Ni vizuri sana kama akibaki, lakini wanakuwa... Leo Messi, Luis (Suarez)... ni wachezaji wakubwa, wanaibadilisha LaLiga.

"Ni zaidi ya miaka 90 ya historia ya LaLiga na nyota wakubwa wamekuwa hapa, na wataendelea kuwapo hapa.

"Lakini mwisho wa siku, kitakachobaki hapa ni LaLiga, na timu ndio kitu muhimu zaidi."

# Man City yawafungia kazi Haaland, Martinez

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, wanaongoza kwenye orodha ya wanaowaniwa na Manchester City kipindi kijacho cha dirisha la usajili, kwa mujibu wa 90min.

Man City inataka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji msimu ujao, huku Haaland na Martinez wakiripotiwa kumuwania kwa udi na uvumba.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya England wanataka kuimarisha safu hiyo ya ulinzi wakati majaliwa ya mshambuliaji Sergio Aguero, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu haujulikani.

Na nyota hao wawili wa Ulaya ndio wanaoongoza kwenye orodha hiyo ya wanaowaniwa pale kwenye dimba la Etihad.

Haaland na Martinez wamekuwa wakihusishwa sana kutua Real Madrid na Barcelona.

Ripoti zinasema kwamba majaliwa ya Aguero hayajulikani huku Gabriel Jesus ndiye akionekana kubeba mikoba ya ushambuliaji pale City.

Haaland msimu huu ana mabao manne kwenye Ligi Kuu ya mabingwa Ulaya.

Martinez ana bao moja na pasi za mwisho tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku aktengeneza nafasi tano.







# *Suarez: Atletico Madrid itafanya makubwa*

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Atletico Madrid, Luis Suarez, amesema yeye na wachezaji wenzake wana imani timu inaweza kupata "mafanikio makubwa" msimu huu.

Suarez aliondoka Barca kwenda kujiunga na Atletico mwanzoni mwa msimu huu wa 2020-21 na raia huyo wa Uruguay ameisaidia timu hiyo kubaki kuwa timu pekee ambayo haijafungwa kwenye LaLiga msimu huu.

Atletico imeshinda mechi tano za ufunguzi kati ya saba wakipitwa pointi mbili na vinara Real Sociedad, ambao wamecheza mechi mbili zaidi.

Kikosi hicho cha Diego Simeone, Atletico – kilimaliza nafasi ya pili mwaka 2014 na 2016 – pia kipo nafasi ya pili kwenye Kundi A la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakipitwa pointi tano na vinara Bayern Munich.

Suarez amefunga mabao matano kwenye LaLiga – sawa na Joao Felix pale Atletico na ameelezea maisha yake pale Madrid, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameliambia gazeti la Marca Sport: "Nafurahia sana.

"Timu ya Atletico iko vizuri na imeunganika na naamini tutaweza kufanya mambo makubwa sana msimu huu."

## De Boer afurahia ushindi wa kwanza Uholanzi

**AMSTERDAM,** Uholanzi

FRANK de Boer alikuwa na furaha kumaliza kipindi cha kusubiri ushindi wake wa kwanza kama kocha wa Uholanzi wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Bosnia-Herzegovina kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Baada ya kuchukua nafasi ya Ronald Koeman katika kikosi hicho, De Boer alicheza mechi nne bila ushindi kabla ya kupata mafanikio Jumapili pale Amsterdam.

Georginio Wijnaldum alikuwa mchezaji wa kwanza tangu Tonny van der Linden mwaka 1961 kufunga mabao mawili katika kipindi cha dakika 13 kwa Uholanzi, kabla ya Memphis Depay kufanya matokeo kuwa 3-0.

De Boer alionyesha kufurahishwa na ushindi huo, huku sasa kikosi chake kikiwa nyuma ya Italia kikipitwa pointi moja na mchezo mmoja ukiwa umebaki kwenye kundi hilo la A1.

"Bila shaka mara zote unakuwa unasubiri kwa hamu kubwa kupata ushindi wa kwanza," alisema.

"Lakini tukajaribu kusubiri na mwisho wa siku mambo yakawa mazuri na sasa tumepata ushindi wetu wa kwanza."



# MASCHERANO ATUNDIKA DALUGA



**BUENOS AIRES,** Argentina

NYOTA wa zamani wa Barcelona, Liverpool na Argentina, Javier Mascherano, ametangaza kustaafu soka.

Mascherano mwenye umri wa miaka 36, alitangaza maamuzi hayo Jumapili, baada ya kucheza soka kwa kipindi cha miaka 17.

Akiwa amecheza mechi 147 kwa timu ya Taifa ya Argentina, akishikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi katika historia ya nchi hiyo, Mascherano alirudi katika klabu yake ya zamani ya Estudiantes de La Plata, Januari.

Baada ya kucheza mechi 11 katika mashindano yote kwenye kikosi hicho cha Argentina, ukiwamo mchezo wa Jumapili wa kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Argentinos Juniors, Mascherano alisema ni muda wake sasa kutundika daluga.

"Nataka kutangaza leo kuwa nastaafu rasmi kucheza soka la kulipwa," alisema.

"Nataka kuishukuru klabu hii ambayo ilinipa mimi nafasi ya kumalizia kipindi changu cha uchezaji hapa Argentina."

Mascherano aliongeza: "Nimecheza soka la kulipwa kwa asilimia 100, nashukuru kwa hilo.

"Leo, nimeona kwamba huu ndio wakati muafaka kwa mimi kustaafu soka rasmi. Asante sana Estudiantes, ambao mliniamini nilipoamua kurudi Argentina."

# *Henderson aongeza majanga Liverpool*

**LONDON,** England

JORDAN Henderson alitolewa wakati England ikikubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Ubelgiji baada ya kuumia, hivyo kuongeza majeruhi katika kikosi cha Liverpool.

Nahodha huyo wa 'Wekundu' hao wa Anfield, Henderson alitolewa kwenye mchezo huo pale Den Dreef, wakati wakichezea kichapo kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Kocha wa England, Gareth Southgate, alithibitisha Henderson alitolewa nje kwa sababu ya kuumia misuli.

"Jordan hakuwa fiti kwa kipindi cha pili na alionekana kwamba hasingeweza kuendelea kucheza," alisema. "Pengine timu ya madaktari ndio wanaoweza kutoa taarifa baada ya kufanya uchunguzi wa kimatibabu."

Liverpool itacheza na Leicester City wakati itakaporudi kwenye Ligi Kuu, huku tayari wakiwa wanakabiliwa na majeruhi kwenye safu yao ya ulinzi.

Jurgen Klopp anaweza kuwa bila ya mlinzi wake wa kati chaguo la kwanza, Joe Gomez ambaye alifanyiwa upasuaji wa goti wiki iliyopita, akiungana na Virgil van Dijk ambaye atakuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Hiyo inamaana kwamba, Fabinho naye hatakuwapo kwenye kikosi cha Liverpool kutokana na majeruhi, huku pia Thiago Alcantara akiwa bado hajacheza mchezo wowote hadi sasa kutokana na majeraha.

Trent Alexander-Arnold anakabiliwa na uwezekano wa kukaa nje ya dimba kwa kipindi cha mwezi mmoja, huku pia Mohamed Salah akikutwa na virusi vya corona na hivyo anatakiwa kujitenga kwa muda.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE ATETA KUBAKI MAN CITY

●●● Ningependa kubaki klabuni hapa, ni rahisi, kama nisingetaka ningeshazungumza na...

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Kevin De Bruyne, amesema anataka kubaki kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya England, wakati akizungumzia kuhusu hali ya mkataba wake kwa sasa.

**Majaliwa ya De Bruyne yamekuwa yakijadiliwa sana, na sasa City wanaangalia uwezekano wa kumwongezea mkataba wa miaka mitano mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliwasili hapo kwenye dimba la Etihad akitokea Wolfsburg mwaka 2015 - na mkataba wake wa sasa kwa kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola unamalizika mwaka 2023.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa yake baada ya Ubelgiji kushinda kwa mabao 2-0 kwenye Ligi ya Mataifa ya UEFA dhidi ya England Jumapili, De Bruyne aliiambia VTM Nieuws: "Nipo kwenye klabu nzuri pamoja na wamiliki wazuri.

"Tupo kwenye mazungumzo - hayajasonga sana mbele. Kwa sasa mimi mwenyewe ndio nafanya mazungumzo.

"Ningependa kubaki klabuni hapa, ni rahisi, kama nisingetaka kubaki, ningeshazungumza na mtu mwingine haraka. "Lakini ukitaka kubakia, si kitu kigumu."

Tangu alipojiunga na City miaka mitano iliyopita, De Bruyne ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu, manne ya EFL, FA na Ngao ya Jamii.

Katika mechi 161 alizocheza kwenye Ligi Kuu England, De Bruyne ameshinda mechi 110, akipoteza 23, mabao 37 na pasi za mwisho 69 kwa City.

Msimu huu, De Bruyne amefunga bao moja na pasi za mwisho tatu na Man City wapo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, wakipitwa pointi sita na vinara Leicester City, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

## ZISIKUPITE

### POGBA HALI TETE UNITED

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, anasema kwa sasa anapitia kipindi kigumu sana pale kwenye dimba la Old Trafford. ***(RTL via Goal)***

### HAKAN HUYOOO ATLETICO

KIUNGO wa AC Milan, Hakan Calhanoglu, mwenye umri wa miaka 26 raia wa Uturuki, huenda yuko njiani kuelekea Atletico Madrid baada ya mazungumzo ya mkataba na klabu hiyo ya Italia kushindikana, ingawa Manchester United bado wanamtaka. ***(Mundo Deportivo)***

### BAKAYOKO KUUZWA

KLABU ya Chelsea tayari imekwisha kubali mkataba wa kumuuza kiungo wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko, mwenye umri wa miaka 26, kwa Napoli wakati uhamisho wake wa mkopo utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Gazetta Dello Sport via Teamtalk)***

### RUDIGER AIFIKIRIA BARCA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger, mwenye umri wa miaka 27, yuko makini kuhusu kujiunga na klabu ya Barcelona wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa Januari. ***(Sport via Metro)***

### DAYOT ATABIRIWA BAYERN

KOCHA wa zamani wa RB Leipzig, Ralf Rangnick, anaamini mlinzi wa kati, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, ambaye Liverpool wanamlenga kumchukua, anaweza kupata mafanikio kule Bayern Munich. ***(Goal)***

### JUVE KWA GRAVENBERCH

KLABU ya Juventus ipo tayari kumnunua nyota mchanga anayechezea Ajax, Ryan Gravenberch, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona katika mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 tu. ***(Tuttosport)***

### ATUMWA KWA BARKLEY

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Aston Villa, Kevin Phillips, anaamini kuwa kocha Dean Smith anapaswa kumshawishi Ross Barkley mwenye umri wa miaka 26, anayecheza kwa mkopo klabuni hapo ili kusaini mkataba wa kudumu. ***(Birmingham Mail)***

### BREMER SASA AGOMBEWA

KLABU za Liverpool na Everton zipo kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Brazil, anayechezea Torino, Gleison Bremer mwenye umri wa miaka 23. ***(Liverpool Echo)***

### WAKALA AIONYA UNITED

MANCHESTER United imeonywa na wakala wa Eric Bailly kwamba mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ivory Coast, huenda akafikiria upya mustakabali wake kama hali ya sasa ya kutopata nafasi ya kucheza haitabadilika. ***(Calciomercato via the Sun)***

### FERNANDES KUUZWA JANUARI

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, amesema mkataba wa mkopo wa kiungo Gedson Fernandes, mwenye umri wa miaka 21, kutoka Benfica unaweza kufikia kikomo Januari. ***(Sport TV via Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Gwambina kuongeza watatu dirisha dogo

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI dirisha dogo la usajili Tanzania Bara likitarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, timu ya Gwambina FC, inatarajia kuongeza wachezaji watatu, imeeleza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Fulgence Novatus (pichani), alisema wachezaji atakaowaongeza watasaidia kuziba nafasi ambazo amebaini kuna mapungufu.

"Katika usajili wa dirisha dogo, nina mpango wa kuongeza wachezaji watatu au wanne ili kuiongezea nguvu timu yangu," alisema.



Alisema anaamini wachezaji watakaowaongeza wataisaidia timu yake isishuke daraja licha ya msimu huu kuwa na ushindani mkubwa.

Kocha huyo, ambaye timu yake ipo nafasi ya tisa ikiwa na pointi 14 baada ya michezo 10, alisema hawatasajili kutokana na jina la mchezaji bali ubora na kiwango ndicho watakachokiangalia muda ukifika.

## Sembi aipa TPC ubingwa Gofu

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZA Gofu, George Sembi wa TPC, amefanikiwa kubakiza ubingwa nyumbani baada ya kuibuka kinara katika mashindano ya wazi ya TPC yaliyomalizika mwishoni mwa wiki Moshi mkoani Kilimanjaro.

Mchezaji huyo aliibuka na ushindi huo baada ya kupiga mikwaju 147 akifuatiwa na Vicent Gulo wa TPC waliyefungana na Isihaka Daudi wa Lugalo ambaye ameshika nafasi ya tatu kwa mikwaju yake 149.

Kwa upande wa Divisheni A, mshindi ni Nahuum Gabriel aliyepata mikwaju 147 akifuatiwa na Juma Mcharo aliyepiga mikwaju 148 huku Divisheni B, mshindi akiwa ni Private Laurent Sangawe kwa mikwaju 149 akifuatiwa na Private Haridi Shemdolwa wote wa Lugalo baada ya kupata mikwaju 152.

Divisheni C, mshindi ni Sahif Kanabhai wa Arusha baada ya kupiga mikwaju 154 akifuatiwa na Issa Issa wa TPC kwa mikwaju 147.

Kwa upande wa wanawake mshindi ni Madina Iddi kwa mikwaju 146 akifuatiwa na Neema Ulomi wote hao ni wa Arusha, huku kwa wazee Ashik Nanabhai wa Arusha akiibuka mshindi na kwa upande wa watoto viwanja tisa, mshindi ni Zacharia George na viwanja 18 mshindi ni Ibrahim Gabriel kwa mikwaju 145.

# NTIBAZONKIZA WA YANGA AZIDI KUNOGA NA BURUNDI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM wanaodhamini Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said, akisema nyota wao mpya waliyemsajili, Said Ntibazonkiza, anatarajiwa kuanza kutumikia rasmi klabu hiyo baada ya kumalizika kwa ratiba ya Kalenda ya Fifa wiki hii, straika huyo amezidi kutisha nyavuni.

**Wiki iliyopita, Injinia Hersi alisema mkataba rasmi wa mchezaji huyo baada ya mechi za kimataifa kumalizika wiki hii na baada ya hapo atatua nchini kujiunga na klabu yake mpya ya Yanga.**

Yanga ilimsajili Ntibazonkiza baada ya mechi ya kimataifa ya kirafiki kati ya Stars na Burundi, ambayo ilimalizika kwa mshambuliaji huyo kuwabebesha Warundi ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo huo uliopigwa Oktoba 11, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Lakini hata kama Ntibazonkiza atatua na kujiunga na timu hiyo, itabidi kuendelea tu kujifua na wenzake hadi dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa Desemba 15, mwaka huu, ili kukamilisha taratibu zote.

Hata hivyo, wakati huu akiwa na timu yake ya Taifa ya Burundi kwenye mechi za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022, Ntibazonkiza amezidi kuonyesha kwamba Yanga haikukosea kumsajili kutokana na kasi yake ya kucheka na nyavu.

Ntibazonkiza ambaye ni kiungo mshambuliaji, amefumania nyavu kwenye mechi mbili mfululizo za kuwania kufuzu Afcon nchini Cameroon 2022.

Katika mechi ya juzi ambayo Burundi ilishinda 3-1 dhidi ya Mauritania, Ntibazonkiza alicheka na nyavu mara mbili, moja akionyesha ubora wake kwa mpira 'uliokufa' wa [adhabu ndogo] nje kidogo ya 18 na la pili akitupia wakati akiwa ndani ya boksi.

Mabao hayo mawili yanamfanya straika huyo kuifunga Mauritania mara tatu, ambapo moja aliwafunga kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Novemba 11, mwaka huu.

Ntibazonkiza sasa anatarajiwa kuonyesha tena ubora wake nyavuni Novemba 22, mwaka huu, wakati Burundi itakapowakaribisha Jamhuri ya Afrika ya Kati kwenye kinyang'anyiro hicho cha kuwania kufuzu AFCON 2022.

UMETISHA...



Rais wa TFF, Wallace Karia (kulia), akimpongeza bondia Hassan Mwakinyo baada ya kumdunda Muargentina Jose Carlos Paz na kutwaa ubingwa wa Mabara wa WBF uzito wa Super Welter, pongezi hizo alizitoa wakati wa hafla fupi iliyoandaliwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salam jana, kwa ajili ya kumpongeza bondia huyo pamoja na timu ya Taifa ya Wanawake U-17 kwa kutwaa ubingwa wa COSAFA. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## *Yanga, Azam zatawala rekodi Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kuongoza Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa na kushika nafasi ya pili, timu za Azam FC na Yanga zimekuwa na rekodi nyingine safi, moja ikiiongoza kupata pointi nyingi nyumbani na nyingine ugenini.

Mpaka kufikia raundi ya 10 ya Ligi Kuu ambapo kwa sasa imesimama kupisha mechi za kimataifa, Azam FC ambayo inaongoza mpaka sasa ikiwa na pointi 25, ndiyo timu inayoongoza pia kupata pointi nyingi ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, Azam Complex.

Azam imezoa jumla ya pointi 16 nyumbani, ikicheza mechi sita, ikishinda tano na kutoka sare moja ambayo ilikuwa ni ya mabao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania.

Timu hiyo imecheza mechi nne ugenini na kuokota pointi tisa, ikishinda tatu na kufungwa moja. Ikumbukwe Azam ilipoteza mechi yake dhidi ya Mtibwa Sugar kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Wakati Azam ikivuna pointi nyingi nyumbani, Yanga ndiyo timu inayoongoza kwenye Ligi Kuu kwa kuzoa pointi nyingi ikiwa ugenini. Imeshakusanya pointi 13 mpaka sasa. Imecheza mechi tano ugenini, ikishinda nne na kutoka sare moja. Mechi ambayo ilitoka sare ilikuwa dhidi ya Gwambina, ilipolazimishwa sare ya bila kufungana.

Yanga pia imecheza mechi tano ikiwa nyumbani, lakini imekusanya jumla ya pointi 11 tu, ikishinda tatu na kutoka sare mbili. Mechi ambazo ikitoa sare ni ya bao 1-1 dhidi ya Prisons na sare kama hiyo dhidi ya Simba Novemba 7, mwaka huu.

# Michezo

Jumanne Novemba 17, 2020

Nipashe




De Bruyne ateta kubaki Man City UKURASA 22

HUPATI KITU...



Mshambuliaji wa England, Harry Kane, akijaribu kufunga huku kipa wa Ubelgiji, Thibaut Courtois, akiwa makini kusoma mwelekeo wa mpira wakati wa mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya iliyopigwa kwenye Uwanja wa King Power juzi usiku na kumalizika kwa England kuchapwa 2-0, mabao yakifungwa na Youri Tielemans na Dries Mertens. **PICHA: MTANDAO**

## Kaze sokoni Yanga kusaka mastraika

**Na Saada Akida**

WAKATI dirisha dogo la usajili likitarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema atasajili 'majembe' ya uhakika katika safu yake ya ushambuliaji yatakayoweza kuwatesa mabeki wa timu pinzani.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya African Lyon juzi usiku waliyoibuka na ushindi wa mabao 3-1, Kaze alisema kwa kipindi kifupi alichokaa na timu hiyo amebaini mapungufu hasa kwenye safu ya ushambuliaji kushindwa kuwa na makali.

Alisema kikosi chake kipo vizuri katika idara zote, lakini kinampa changamoto katika safu ya ushambuliaji ambayo inakosa watu wakuweza kuwasumbua mabeki wa timu pinzani.

"Tumekuwa tunashinda mechi zetu, lakini bado hatua watu ambao wanaweza kutia presha kwa wapinzani, tunahitaji kupata watu mbele watakaoweza kupambana kutafuta matokeo," alisema.

"Katika mechi nyingi ikiwamo hii ya kirafiki dhidi ya African Lyon, nimeona jinsi gani washambuliaji wangu wanavyopokonywa mipira na mabeki, hili nalifanyia kazi kwa kipindi hichi, lakini bado nahitaji wachezaji wapambanaji watakaowasumbua mabeki wa timu wapinzani," alisema kocha huyo.

Hadi sasa safu ya ushambuliaji ya Yanga imefunga mabao 12 baada ya mechi 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara huku mabeki wakiruhusu mabao matatu pekee.

# Stars, Tunisia kuamua AFCON

## ●●● Equatorial Guinea yaongeza ugumu kwa Tanzania, Watunisia wahitaji ushindi kufuzu, lakini...

**Na Saada Akida**

NI ushindi tu! Hicho ndicho Taifa Stars inachokihitaji leo dhidi ya Tunisia, ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022 nchini Cameroon, itakapowakaribisha Watunisia hao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kupigwa bao 1-0 Jumamosi iliyopita dhidi ya Watunisia hao, na ushindi pekee ndio utakaoiweka katika nafasi ya kufuzu kutoka Kundi lao la J, ambalo Tunisia ipo kileleni ikiwa na pointi tisa ikifuatiwa na Equatorial Guinea yenye alama sita baada ya juzi kuichapa tena Libya iliyopo mkiani ikiwa na alama tatu sawa na Tanzania.**

Hivyo, Libya na Equatoria Guinea zenyewe zimeshacheza mechi nne, wakati Taifa Stars na Tunisia leo ndio zitakamilisha raundi yao ya nne.

Tunisia inahitaji ushindi ili kufuzu fainali hizo, ambazo kwa Stars kama ikifuzu, itakuwa ni mara ya tatu katika historia ya Tanzania kushiriki michuano hiyo mikubwa zaidi barani Afrika.

Tayari Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita, na anaamini kujituma kwa wachezaji ndiyo silaha pekee ya ushindi katika mechi hiyo ambayo kiingilio cha chini ni Sh. 5, 000 huku VIP A kikiwa Sh. 20,000 tu.

"Tunisia ni timu kubwa, lakini tutakuwa nyumbani na vijana wangu naamini wataipambania bendera ya taifa, ukibeba bendera ya taifa lazima ujitolee, tumeamua kujitoa hii ni timu ya taifa kila mtu lazima ajitolee," alisema kocha huyo raia wa Burundi, huku akiwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao kwenye mechi hiyo itakayopigwa majira ya saa nne usiku.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Idara Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema kulingana na mabadiliko ya muda wa mchezo huo, idadi ya mashabiki watakaowaruhusu kuingia kushuhudia ni 20,000 tu.

Alisema idadi hiyo ya mashabiki inatokana na utaratibu uliowekwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), katika kipindi cha hiki cha kupambana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

"Mashabiki wanatakiwa kuzingatia sheria na maagizo ya CAF kuhusu utaratibu, ni kukaa umbali kidogo, ninaimani Watanzania watazingatia hilo ili tuweze kupata fursa hiyo kwa klabu zetu za Simba na Namungo ambazo zinaiwakilisha nchini kwenye michuano ya kimataifa," alisema Singo huku akisisitiza kuhusu usalama kila kitu kipo vizuri.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema walijaribu kuomba mechi hiyo isichezwe usiku wa saa 4:00, badala yake muda urudishwe nyuma na kuwa saa 1:00 au saa 2:00 usiku, lakini CAF ilikataa.

"Tuliongea CAF walikataa wakitoa sababu kuwa haki ya matangazo ya televisheni inawabana na isingewezekana kwa mechi hiyo kuchezwa saa 1:00 au saa 2:00," alisema Kidau.

Kwa upande wa Kamati ya Hamasa ya Saidia Stars ishinde, Katibu wa Kamati hiyo, Injinia Hersi Said, alisema: "Tutahakikisha tunawapa sapoti vijana na kuanzia hapa tutasimamia kila kitu na kuna kitu kizuri na kikubwa zaidi tumewaandalia kama watashinda."

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Haji Manara, alisema: "Inapofika suala la timu ya Taifa hakuna visingizio, hivyo hakuna shabiki wa Simba, Yanga, Kagera na timu zote, wote tunakuwa ni Taifa Stars. Akishika mpira Bocco, Feisal na wengine wote basi tushangilie kwa pamoja".

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >